SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ILIYOSOMWA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI NA WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS, KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI

MHE. SHARIFF ALI SHARIFF (MBM)



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi akipata maelezo kutoka kwa Mwenyekiti na Muekezaji wa Hoteli ya nyota tano ya Zanzibar Crown Hotel and Resort Limited Bw. Nadhim Rawahiil iliyopo Mazizini, Mkoa wa Mjini Magharibi
Tarehe: 07 Januari 2024

***"Tuimarishe mazingira ya kazi kwa kuleta ufanisi katika Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi"***

***MEI, 2024***

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## AFISI YA RAIS KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ILIYOSOMWA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHINA WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS, KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI

MHE. SHARIFF ALI SHARIFF (MBM)

MEI, 2024



MHE. SHARIFF ALI SHARIFF (MBM)

WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS, KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI
ZANZIBAR.

## YALIYOMO


VIFUPISHO VYA MANENO ..... v

HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ..... 1

1.0 UTANGULIZI ..... 1

2.0 MIKAKATI YA KUKUZA SEKTA YA KAZI, UWEZESHAJI NA UWEKEZAJI. ..... 5

2.1 UKUAJI WA SEKTA YA KAZI, UWEZESHAJI NA UWEKEZAJI ..... 6

3.0 MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA UTATUZI WA CHANGAMOTO KATIKA SEKTA YA KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI. ..... 12

3.1 MAFANIKIO ..... 12

3.2 CHANGAMOTO ..... 18

3.3 UTATUZI WA CHANGAMOTO ..... 18

4.0 MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023. ..... 20

4.1 MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KWA FUNGU A07 (KAZI NA UWZEZESHAJI). ..... 21

4.2 MUHTASARI WA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI, 2023 - MACHI, 20244.2.1 FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI). ..... 22

4.3 MUHTASARI WA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI, 2023 - MACHI, 2024. FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI). ..... 25

5.0 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 ..... 26

6.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI). 29

6.1 PROGRAMU KUU PA0702: USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI KAZI NA KAZI ZA STAHA KWA WOTE. 29

6.1.1 Programu ndogo: SA070201. Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha. 29

6.1.2 Programu Ndogo SA070202: Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini. 32

6.1.3 Programu Ndogo SA070203: Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini. 34

6.2 PROGRAMU KUU PA0703: UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI. 39

6.2.1 Programu Ndogo: SA070301: Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi 39

6.2.2 Programu Ndogo: SA070302: Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika. 43

6.2.3 Programu ndogo SA070303: Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. 46

6.3 PROGRAMU KUU PA0705: UENDESHAJI NA URATIBU WA OFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI. 54

6.3.1 Programu ndogo SA070501: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi. 55

6.3.2 Programu ndogo SA070502: Utawala na Uendeshaji. 59

6.3.3 Programu ndogo SA070503: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba. 61

7.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI) 66

7.1 PROGRAMU KUU: PA0801 KUIMARISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI. 66

7.1.1 Programu ndogo SA080101: Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. 67
7.1.2 Programu ndogo SA080102: Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji. 69
7.2 PROGRAMU KUU PA0802: UENDESHAJI NA URATIBU WA OFISI KATIKA UCHUMI NA UWEKEZAJI. 73
7.2.1 Programu ndogo SA080201: Utawala na Uendeshaji. 73
7.2.2 Programu ndogo SA080201: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi. 75
7.2.3 Programu ndogo SA080203: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba. 76
8.0 MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025. 80
8.1 VIPAUMBELE VYA AFISI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 80
9.0 MUELEKEO WA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025. 81
9.1 MAPATO 81
9.2 MATUMIZI 81
10.0 MUELEKEO WA MATUMIZI KWA KILA PROGRAMU 85
10.1 FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI) 85
10.2 FUNGU A11 WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI 92
10.2.1 Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wakala Pemba 95
10.3 FUNGU A08 UCHUMI NA UWEKEZAJI 97
10.3.1 MUELEKEO WA MATUMIZI KWA KILA PROGRAMU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI). 98
11.0 SHUKURANI. 103
VIAMBATANISHO 106
UKUAJI WA SEKTA YA UWEZESHAJI, UWEKEZAJI NA KAZI 106
FEDHA ZILIZOTOLEWA NA WANUFAIKA KUPITIA MKOPO

WA INUKA JULAI, 2023 – MACHI, 2024 ..... 107
MAREJESHO YA MIKOPO KUPITIA PROGRAMU 3 KUANZIA JULAI 2023 - MACHI 2024 ..... 109
FEDHA ZA PROGRAMU YA MAKUNDI MAALUM (4:4:2) ZILIZOPOKELEWA KUTOKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA. ..... 111
IDADI YA VYAMA VYA USHIRIKA VILIVYOSAJILIWA ..... 113
MUHTASARI WA MAPATO YALIYOKUSANYWA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 ..... 117
MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI NA MATUMIZI KWA MISHAHARA, RUZUKU, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI, 2023 – MACHI, 2024 ..... 118
TANBIHI ..... 119
MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI NA MATUMIZI KWA KIPINDI JULAI 2023-MACHI 2024 (FUNGU A07) ..... 120
MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI NA MATUMIZI YA MISHAHARA, RUZUKU, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2023-MACHI 2024 ..... 122
MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI NA MATUMIZI KWA KIPINDI JULAI 2023-MACHI 2024 (FUNGU A08) ..... 123
PROGRAMU KUU NA NDOGO ZA AFISI YA RAIS, KAZI,UCHUMI NA UWEKEZAJI KWA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI), FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI) NA FUNGU A11 (UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI) ..... 124
MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ..... 126
MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 KWA FUNGU A07 ..... 129
MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 FUNGU A11 ..... 130
MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 FUNGU A08 ..... 131

# VIFUPISHO VYA MANENO

ADB: Benki ya Maendeleo ya Afrika.
ARKUU: Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji.
BOA: Bank of Afirica: Benki ya Afrika.
COSTECH: Commission for Science and Technology (Tumeya Sayansi na Teknolojia).
CRDB: Cooperative and Rural Development Bank (Benki ya Maendeleo ya Ushirika.
CSR: Corporate Social Responsibility.
DTB: Diamond Trust Bank.
FAO: Food and Agriculture Organization (Shirika la Kimataifa la Kilimo na Chakula).
ILO: International Labour Organization (Shirika la Kazi Duniani).
JKU: Jeshi la Kujenga Uchumi.
KCB: Kenya Commercial Bank (Benki ya Biashara ya Kenya).
NEET: Not in Education, Employment and Training (Vijana Wasio kwenye Ajira, Elimu na Mafunzo).
PBB: Program Based Budget (Bajeti inayotumia Mfumowa Programu)
PBZ: People’s Bank of Zanzibar (Benki ya Watu wa Zanzibar).
PDB: Presidential Delivery Bureau (Taasisi ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Mheshimiwa Rais)

| | |
|---|---|
| SMIDA: | Small and Medium Industrial Development Agency (Wakala wa Viwanda Vidogo vidogo na vya Kati). |
| TEHAMA: | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TCB: | Tanzania Commercial Bank (Benki ya BiasharaTanzania). |
| UNDP: | United Nations Development Program (Shirika laKimataifa la Maendeleo) |
| ZANEMA: | Zanzibar Employer Association (Jumuiya ya WaajiriZanzibar). |
| ZATUC: | Zanzibar Trade Union Congress (Shirikisho laWafanyakazi Zanzibar). |

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZIKWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 AFISI YA RAIS,KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI.

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja kwa Baraza lako likae kama Kamati ya Matumizi ili iweze kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote nachukua fursa hii adhimu kumshukuru Allah (Subhanahu Wataala) kwa Rehma zake na kwa kutujaalia Afya njema, Amani, na utulivu katika Nchi yetu. Aidha, namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie busara na uwezo zaidi wa kuweza kufanya kazi na kutekeleza majukumu yetu ipasavyo ili kuleta maendeleo ya Nchi.

3. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kunipa heshima kubwa na kuniamini kwa kuniteua kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji. Naahidi kwamba nitamsaidia na nitajitolea kwa nguvu zangu zote katika utekelezaji wa majukumu yangu na kuleta maendeleo makubwa katika sekta ya Kazi, Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Nchini.

4. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, kwa nafasi ya kipekee napenda kuchukua fursa hii kutoa mkono wa pole kwa

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuondokewa na baba mzazi Al Hajj Ali Hassan Mwinyi ambae pia ni Rais mstaafu wa Awamu ya Tatu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ni mlezi wa Taifa letu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amuweke marehemu mahali pema na ampe subira Mheshimiwa Rais na familia yake katika kipindi hichi cha huzuni na ampe nguvu katikakuliongoza Taifa letu. Vilevile, napenda kuchukua fursa hii kutoa mkono wa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na Rais Mstaafu wa Awamuya Pili wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Al Hajj Ali Hassan Mwinyi. Sambamba na hilo natoa pole kwa kuondokewa na aliekuwa Waziri Mkuu Mstaafu Nd. Edward Ngoyai Lowassa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema roho za viongozi wetu na awape Subira Wafiwa na Watanzania wote hasa katika kipindi hiki cha huzuni.

5. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii adhimu kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mafanikio makubwa alioyapata katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 na Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Aidha, Katika kipindi hiki, wananchi wa Zanzibar wameshuhudia maendeleo makubwa hasa katika kuimarisha uwekezaji na uwezeshaji, jambo ambalo linaibua upatikanaji wa fursa za ajira kwa wananchi na kuchangia katika ukuaji wa uchumi Zanzibar ambapo kwa hivi sasa umekua kwa asilimia 0.3 kutoka asilimia 6.8 mwaka 2022 hadi asilimia 7.1 mwaka 2023.

6. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, nazipongeza juhudi za Mheshimiwa Rais za kufuatilia kwa karibu utendaji wa Taasisi za Serikali kupitia maagizo, maelekezo, ziara na majadiliano ya ana kwa ana na watendaji wa Serikali, Taasisi ya Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Vipaumbele vya Mheshimiwa Rais (PDB) pamoja na Mfumo wa Sema na Rais (SNR- Mwinyi). Hatua hizo zimeendelea kuimarisha ufanisi katika utendaji, uwajibikaji, usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wa majukumu ya Wizara na Taasisi za Serikali pamoja na utatuzi wa changamoto zinazowakabili wananchina wafanyakazi katika sekta yetu.

7. **Mheshimiwa Spika,** Pia, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyikwa juhudi za pamoja wanazochukua katika kukuza uchumi wa Nchi, ikiwemo kutangaza vivutio na fursa za uwekezaji zilizopo Tanzania pamoja na kusisitiza kudumisha amani na utulivu uliopo. Sambamba na hilo, nawapongeza kwa juhudi zao za dhati za kusimamia masuala ya kidiplomasia yanayopelekea kuimarisha mashirikiano mema na mazuri baina ya Nchi yetu na mataifa mbali mbali duniani yanayosaidia kukuza uchumi wa nchi yetu.

8. **Mheshimiwa Spika,** Nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuweka Saini miswada minne ya Sheria ikiwemo Sheria ya Uwekezaji Zanzibar namba 10 ya mwaka 2023, pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria ya Ajira namba 11 ya mwaka 2005, jambo ambalo linaweka

mazingira mazuri ya kazi na uwekezaji zinazopelekea ukuaji wa Uchumi wa Zanzibar. Pia, tunatoa pongezi za dhati kwa kuadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mafanikio makubwa. Maadhimisho hayo yalikuwa ni ya kipekee ambapo imeonesha ukomavu wa Nchi na hali halisi ya maendeleo.

9. **Mheshimiwa Spika,** Nawapongeza kwa dhati Viongozi Wakuu wa Kitaifa Makamu wa Kwanza wa Rais, MheshimiwaOthman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Mhandisi Zena Ahmed Said kwa kufanya kazi bega kwa bega na Mheshimiwa Rais katika kumsaidia na kumshauri masuala mbali mbali ya kuimarisha Umoja, Mshikamano, Amani nakuiletea Maendeleo Nchi yetu.

10. **Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Wafanyakazi wa Afisiya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji napenda kukushukuru Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Utalii, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Mtumwa Peya Yussuf kwa namna unavyosimamia kwa makini kazi za Kamati pamoja na utekelezaji wa majukumu ya Wizara zilizo chini ya Kamati yako kwa lengo la kuleta maendeleo endelevu ya Nchi yetu, chini ya uongozi wako mahiri, hodari na shupavu ambapo shughuli zetu nyingi zimefanikiwa. Pia, nawapongeza Wajumbe wote pamoja na Makatibu wa Kamati kwa kuwa karibu sana na Afisi kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yetu. Aidha, napenda kumshukuru Mwenyekiti, Wajumbe pamoja na Makatibu wa Kamati ya Bajeti na Uchumi ya Baraza la Wawakilishi

ambao walituunga mkono na kuwa nasi bega kwa bega katika kutoa miongozo na maelekezo kwa utendaji wa kazi za Afisi wakati Afisi ilipokuwa chini ya Kamati hiyo.

11. **Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru kwa dhati Mhe. Mudrik Ramadhan Soraga aliekuwa Waziri katika Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa uongozi wake mahiri aliokuwa nao katika kipindi chote cha uongozi katika Ofisi hiyo. Miongozo na maelekezo yake yalipelekea kuimarisha utendaji wa Wizara ambapo masuala ya Uwezeshaji na Uwekezaji yameimarika na kukuza masuala ya ajira na kazikwa wananchi wa Zanzibar.

12. **Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, napenda kushukuru watendaji wa Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji pamoja na wadau wetu wote, kwa mashirikiano makubwa mnayonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kazi. Vile vile, napenda kuchukua fursa hii kuzishukuru Taasisi zote kwa kufanikisha zoezi la ukusanyaji wa takwimu za ajira Nchini. Upatikanaji wa takwimu hizo utasaidia kwa kiasi kikubwa upangaji wa mipango ya maendeleo Nchini pamoja na kuifanyia kazi Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 kuelekea upatikanaji wa ajira laki tatu. Aidha, naishukuru kwa dhati familia yangu kwa kuendelea kunivumilia na kuwa nami bega kwa bega kwa kipindi chote cha Uongozi.

## 2.0 MIKAKATI YA KUKUZA SEKTA YA KAZI, UWEZESHAJI NA UWEKEZAJI.

13. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ina lengo la kuimarisha hali ya kijamii na kiuchumi

ya Wananchi wa Zanzibar kwa kutoa na kutumia fursa za kiuchumi zilizopo na zitakazokuja, kushajihisha utamadunina uwezo wa ujasiriamali, kukuza uwekezaji wa ndani na nje, upatikanaji wa kazi za staha na kuzingatia sheria na viwango vya kazi. Dhamira hii itafikiwa kwa kutekeleza na kuimarisha Sekta ya Uwekezaji, Sekta ya Kazi na Ajira na Sekta ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

14. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji inaendelea kusimamia na kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Ilani ya CCM 2020-2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 (SDGs) na Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Mikakati yote imezingatia kuimarishwa kwa Sekta ya Kazi na Ajira, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Uwekezaji.

## 2.1 UKUAJI WA SEKTA YA KAZI, UWEZESHAJI NA UWEKEZAJI

15. **Mheshimiwa Spika;** Sekta ya Kazi na Ajira inatoa mchango mkubwa wa kujikimu kwa maisha ya wananchi. Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa Mwaka 2020/2021 - Zanzibar unaonesha kwamba kiwango cha ukosefu wa ajira kimeongezeka hasa kwa Vijana kutoka asilimia 21.3 mwaka 2014/2015 hadi asilimia 27.4 mwaka 2020/2021. Hali hii ilichangiwa na Mripuko wa maradhi ya UVIKO-19 yaliyoikumba Dunia. Katika kukabiliana na hali hii, Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji, imeweka mikakati ya Upatikanaji wa Ajira pamoja na kuwawezeshaVijana kuweza kuajirika ikiwemo kuongeza miradi ya Maendeleo na Uwekezaji, kutoa mikopo, mafunzo kwa

wafanya biashara na wajasiriamali na kuwaunganisha na masoko.

16. **Mheshimiwa Spika;** Vile vile, Afisi imeweka mikakati imaraya kuimarisha sekta mbali mbali zinazochangia katika kukuza Ajira. Miongoni mwa mikakati inayowekwa ni pamoja na kufanya mapitio ya Sera na Sheria za Ajira; Kuandaa Mpango Kazi wa Tatu wa Miaka Mitano wa Kuzalisha Ajira; Kuandaa Mswada wa Sheria ya Kukuza Ajira; Kufanya Mapitio ya Mfumo wa Taarifa za Soko la Ajira; Kuimarisha Uwekezaji; Kuandaa programu za kukuza Ajira kwa Vijana na kuimarisha upatikanaji wa takwimu za Ajira Nchini. Aidha, Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na Taasisi ya Ufuatiliaji wa utekelezaji wa vipaumbele vya Mheshimiwa Rais (PDB)imefanya utafiti wa ajira zilizopatikana kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi 2023 na kubainisha kwamba jumla ya ajira 187,651 zimepatikanakupitia sekta za Umma na sekta binafsi.

17. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 upatikanaji wa Ajira rasmi za ndani umeongezeka kwa asilimia 65.9 kutokana na Mikataba inayothibitishwa kutoka ajira 6,348 mwaka 2022/2023 hadi 9,630 mwaka 2023/2024 katika Sekta ya Skuli Binafsi, Hoteli na Viwanda. Aidha, upatikanaji wa ajira nje ya Nchi umekuwa kwa asilimia 285 kutoka ajira 1,080 mwaka 2022/2023 hadi ajira 3,078 kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Ukuaji huu unatokana na kuimarika kwa Sekta ya Uwekezaji Nchini; kuweka mikakati imara ya kusimamia Wakala Binafsi wa Ajira na kuimarika kwa Diplomasia ya Nchi na mataifa mbali mbali ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

imesaini mikataba ya mashirikiano na Nchi ya Qatar, Saudi Arabia na Nchi za falme za Kiarabu kwa lengo la kutoa fursa za ajira kwa Vijana wa kitanzania. Aidha, Serikali inaendelea na majadiliano na Nchi ya Oman, Iraq, Iran na Jordan kwa lengo la kuingia mikataba na nchi mbalimbali. **Kiambatanisho nambari 1(a na b) kinahusika.**

18. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Uwezeshaji ina lengo la kuinua kipato cha mwananchi na mjasiriamali kwa kuwawezesha kupitia mafunzo, mikopo na kuwaunganisha na masoko. Sekta hii imetiliwa mkazo katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 katika Nguzo ya 1 ya Mabadiliko ya Kiuchumi na Mkakati wa Maendeleo wa Zanzibar 2021-2026 pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi Ibara 142 na 143 ambazo zimeweka mikakati ya kuimarisha shughuli za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi hasa katika maeneo ya vipaumbele vya Taifa ikiwemo Sekta ya Huduma, Miundombinu, Utalii, Kilimo na Mifugo na Uchumi wa Buluu.

19. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Uwezeshaji katika kukuza mitaji ya Wajasiriamali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imefanikiwa kutoa mikopo kwa wanufaika 2,045 (Unguja 1224 na 821 Pemba) yenye thamani ya TZS. 7,950,964,141.88 kutoka wanufaika 9,123 mwaka 2022/2023 yenye thamani ya TZS. 15,815,473,033.20 sawa na punguzo la asilimia 77. Hali hii imetokana na Wananchi kutokulipa kwa mikopo hiyo kwa wakati ambapo Asilimia ya mikopo isiyorejeshwa imeongezeka kutoka asilimia 8 kwa mwaka 2022/2023 hadi kufikia asilimia 34 kwa mwaka 2023/2024. Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa

kushirikiana na Benki ya CRDB inaendelea na juhudi za kuratibu urejeshaji wa Mikopo iliotolewa kwa Wananchi. Aidha, Serikali imeimarisha mashirikiano na mabenki ya ndani ikiwemo PBZ, AMANA BENKI, BOA, TADB pamoja na kupata mkopo wa TZS.13 Bilioni kutoka benki ya dunia kwa lengo la kuwapatia wananchi mikopo nafuu kupitia mradi wa PAMOJA. Vile vile, Afisi imekusanya jumla ya TZS
2.1 Bilioni kutoka Mamlaka 11 za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuimarisha utoaji wa mikopo nafuu kwa wananchi kupitia programu ya mikopo kwa makundi maalum ya 4:4:2 (Wanawake 4, Vijana 4 na Watu Wenye Ulemavu 2) **Kiambatanisho nambari 2a (i, ii na iii) kinahusika.**

20. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaimarisha Sekta ya Ushirika ili iweze kuleta ufanisi kutoa ajira, kunyanyua pato la mwananchi na uchumi wa Nchi. Sekta hii inashajiisha uundaji wa vyama vya ushirika kwa lengo la kuwaweka pamoja ili kuweza kupata huduma mbalimbali ikiwemo mafunzo ya ujuzi na mitaji. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imesajili jumla ya vyama 1,560 ikilinganishwa na vyama 1,822 kwa mwaka 2022/2023 sawa na punguzo la asilimia 16.7. Hali hii imetokana na uhaba wa fedha za mikopo zinazotolewa na Programu ya INUKA kupitia benki ya CRDB na kupelekea kutoundwa kwa Vyama vya Ushirika kwa ajili hiyo. Aidha, Serikali inaimarisha uundaji wa Vyama miamvuli kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za mitaji, mafunzo pamoja na ufuatiliaji wa ulipaji wa madeni ya mikopo inayotolewa kupitia mifumo ya kidigitali. **Kiambatanisho nambari 2(b) kinahusika.**

21. **Mheshimiwa Spika,** Katika masuala ya Uwezeshaji, Afisi imepiga hatua katika utoaji wa mafunzo kwa wajasiriamali katika maeneo ya ufugaji wa nyuki, usarifu wa matunda na mboga mboga, utengenezaji wa vifaa vya sola, masoko, ujasiriamali na mafunzo ya uokaji (uokaji) ambapo umeongezeka kutoka wajasiriamali 1,239 kwa mwaka 2022/2023 hadi kufikia 3,979 (Unguja 1963 na Pemba 2,016) kwa mwaka 2023/2024.

22. **Mheshimiwa Spika,** Mbali ya mafunzo ya utafutaji wa masoko, Serikali inawaunganisha wajasiriamali na masoko mbali mbali ya ndani na nje ya Zanzibar kupitia maonesho yakiwemo maonesho ya Afrika Mashariki, Sabasaba na Maonesho ya Mapinduzi, maonesho ya fahari ya Zanzibar na maonesho ya marashi ya karafuu, ambapo idadi ya Wajasiriamali waliounganishwa na masoko imeongezeka kwa asilimia 31 kutoka wajasiriamali 148 mwaka 2022/2023 hadi kufikia wajasiriamali 194 mwaka 2023/2024, hii imetokana na kufanikiwa kufanya Tamasha la "Fahari ya Zanzibar" kwa upande wa Unguja na tamasha la Marashi ya Karafuu kwa upande wa Pemba ambapo imesaidia Wajasiriamali kuonesha na kuuza bidhaa zao, aidha kupatiwa mafunzo ya utumiaji wa fursa za masoko yakiwemo ya kidigitali na fursa za usajili wa biashara zao.

23. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Awamu ya Nane imedhamiria kuimarisha Sekta ya Uwekezaji kuwa ni miongoni mwa Sekta zinazochangia katika ukuaji wa uchumi Nchini. Katika kipindi cha miezi tisa ya mwaka wa fedha wa 2023/2024, miradi 63 ya uwekezaji imesajiliwa yenye thamani ya dola za kimerekani Millioni 1,499 na inatarajia kutoa ajira zipatazo 4,392. Wizara kupitia

Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar imefanikiwa kuvutia wawekezaji wenye hadhi na mitaji mikubwa katika mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, Mamlaka imekusanya Jumla ya TZS. 3,612,236,760.08 kati ya 2,976,285,884.94 ambayo
ni sawa na asilimia 121 ya makadirio. Kwa upande wa matumizi, Mamlaka imetumia Jumla ya TZS 2,107,890,528 sawa na asilimia 60 ya makadiro ya matumizi.

24. **Mheshimiwa Spika,** Mtaji wa Miradi ya Uwekezaji imekuwa kwa asilimia 209.8 kutoka Dola za Kimarekani 714,707,829 Mwaka 2022/2023 hadi Dola za Kimarekani 1,499,730,258 kwa mwaka 2023/2024. Ukuaji huu umechangiwa na kuweka mazingira mazuri ya kisera na kisheria ambapo Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, amesaini Sheria ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji ya Mwaka 2023 ambayo inatoa fursa nyingi kwa wawekazaji na imeshaanza kutumika. Vile vile,Afisi imeimarisha huduma jumuishi za uwekezaji, kuweka mfumo wa kieletroniki unaorahisisha utoaji wa huduma, kuweka ardhi ya akiba kwa uwekezaji, kuimarisha miundo mbinu ya uwekezaji katika Maeneo Huru ya Uwekezaji ikiwemo Fumba, Micheweni na Dunga. **Kiambatanisho nambari 3(a, b na c) kinahusika.**

25. **Mheshimiwa Spika,** Miradi ya Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) Kwa mwaka wa Fedha 2023/2024, jumla ya miradi 17 imepokelewa. Kati ya hiyo, miradi mitano (5) imefanyiwa uchambuzi na kuonekana kukidhi vigezo kwa kuzingatia vipaumbele vya Nchi. Afisi imesimamia utiaji wa saini ya mikataba minne

(4) ya Maridhiano (Concession Agreement), kwa Sekta ya

Mawasiliano, Usafirishaji na Miundombinu yenye thamani ya Dola za Kimarekani 302 Milioni. Aidha, Afisi imeratibu utiaji wa saini wa Hati za Makubaliano (MoU) nne (4) katika Sekta ya Nishati, Sekta ya Mawasiliano na Benki zikiwemoNMB na NBC.

## 3.0 MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA UTATUZI WA CHANGAMOTO KATIKA SEKTA YA KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI.

## 3.1 MAFANIKIO

**26. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Afisi ilipata mafanikio yafuatayo:

1) Imeongeza makusanyo kutoka TZS. 2,730,161,000 kwa mwaka 2022/2023 hadi TZS. 3,948,700,681.8 Kwa mwaka 2023/2024 sawa na asilimia 145 ya makadirio kupitia vyanzo mbalimbali vikiwemo; uthibitishaji wa mikataba ya wafanyakazi wanaoajiriwa ndani na wanaokwenda nje ya Nchi na utowaji wa vibali vya kazi kwa wageni.

2) Imefanya ukaguzi kazi katika maeneo ya kazi 216 (Unguja 141 na Pemba 75) ili kuhakikisha utekelezwaji wa sheria za kazi katika kulinda haki na Maslahi ya wafanyakazi katika sehemu za kazi.

3) Imethibitisha Mikataba ya kazi ya wafanyakazi wazawa 9,624 (Unguja 8,739 na Pemba 885) lengo ni kuhakikisha masharti ya Mikataba hiyo inaendana na viwango vya sheria, kanuni na miongozo ya kazi. Sawa na asilimia 192 ukilinganisha na lengo ya mikataba 5,000 ya mwaka wa 2023/24.

4) Imepokea Migogoro ya kazi 167, na kuitatua migogoro 94 (67 imesuluhishwa na 27 imefanyiwa maamuzi), 60 inaendelea na hatua na 13 imefutwa. Kwa mwaka 2023/24 imesuhuluhisha migogoro kwa asilimia 17 zaidiukilinganisha na mwaka uliopita (2022/23).

5) Imetoa elimu ya Mambo mbali mbali ya taratibu, haki na wajibu wa kazi katika maeneo ya kazi 30 na kurusha vipindi 60 kupitia televisheni na redio ili kuwapa Waajiri, Wafanyakazi na jamii kwa ujumla uelewa juu ya taratibu za Sheria, Kanuni na miongozo inayohusu haki na wajibu katika kazi.

6) Imetoa mafao ya wafanyakazi ikiwemo ubani wa ufiwa kwa wafanyakazi 7 yenye thamani ya Shilingi Milioni Tatu, na Laki Tisa (TZS 3,900,000), mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi 28 yenye gharama ya Shilingi Mulioni Tano na Laki Tano (TZS 5,500,000), posho la likizo kwa wafanyakazi 80 yenye gharama ya Shilingi Milioni Sita na Laki Nane (TZS 6,800,000).

7) Imesajili Chama kipya cha Waajiri kinachohusika na sekta za Ulinzi Private Security Employers Association (ZPSEA) na vyama viwili miamvuli vya Uvuvi na Kilimo cha Mpunga. Aidha, imefanya kikao cha pamoja na Vyama vyote vya Wafanyakazi vilivyosajiliwa kwa lengo la kujadili utendaji kazi wa vyama pamoja na changamoto wanazokabiliana nazo ili kuzitafutia ufumbuzi.

8) Imefanya mkutano wa mashirikiano wa Utatu baina ya Serikali (Kamisheni ya kazi), Wafanyakazi (Shirikisho la vyama vya wafanyakazi – ZATUC) na Waajiri (Jumuiya

ya Waajiri Zanzibar (ZANEMA) kwa lengo la kujadili changamoto za kazi na ajira katika kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi ili kuweka mikakati ya kuzitatua.

9) Kwa kishirikiana na Afisi ya Waziri Mkuu Kazi, imeandaa na kuwasilisha katika Shirika la Kazi Duniani ILO ripoti yaNchi (Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania) inayohusu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya ILO.

10) Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji kwa kushirikiana na Taasisi ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa vipaumbele vya Mheshimiwa Rais (PDB) imeimarisha mashirikiano na Shirika la Kazi Duniani (ILO) ambapo tunaendelea na matayarisho ya Takwimu za soko la ajira (LMIS)na mfumo wa upatikanaji wa ajira za ndani na nje ya Nchi (Job seekers Portal). Vile vile, (PDB) imetayarisha mkakati wa vipaumbele vya Mheshimiwa Rais katika sekta ya kazi uwezeshaji na uwekezaji na kuwakutanisha na Wadau kwa lengo la kuleta maendeleo nchini.

11) Imefanya usajili wa maeneo ya kazi na kutoa vyeti 134 Vyenye thamani ya TZS 217,008,600 Kwa lengo la kuimarisha masuala ya Usalama na Afya Kazini.

12) Imetoa vibali vya kazi kwa wafanyakazi wa kigeni 2,960 sawa na asilimia 148 ukilinganisha na lengo vyenye thamani ya TZS 2,681,471,350 sawa na ongezeko la asilimia 156.7. Hii imetokana na mabadiliko ya sheria katika kuongeza muda wa kibali kutoka mwaka mmoja hadi miaka miwili.

13) Imefanya utafiti wa taarifa za Ajira katika Sekta rasmi na Sekta isiyo rasmi Zanzibar kwa lengo la kupata

takwimu za ajira, kutambua shughuli za kiuchumi na kijamii zinazofanyika Nchini. Matokeo ya awali ya utafiti wa taarifa za ajira kwa sekta rasmi na zisizo rasmi Zanzibar yanaonesha kuwa jumla ya ajira zilizozalishwa kuanzia Novemba, 2020 hadi Septemba, 2023 ni laki Moja, Themanini na Saba elfu, Mia sita na Hamsini na Moja (187,651) ambapo kati ya ajira hizo, Wanaume ni 93,029 (49.6%) na Wanawake ni 94,622 (50.4%).

14) Imeanzisha Dawati la kuratibu usafirishaji wa wafanyakazi wanaokwenda kufanya kazi nje ya Nchi katika Viwanja vya Abeid Amani Karume.

15) Kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) imeanza utekelezaji wa utoaji wa fao la upotevu wa ajira ambapo jumla ya madai 243 yamewasilishwa na baada ya kukaguliwa madai 215 yamethibitishwa kukidhi vigezo kwa malipo.

16) Kuratibu hatua ya utungaji, kusainiwa na kuanza kutumika kwa kanuni 3 zinazosimamia masuala ya kaziikiwemo kanuni ya kuanzisha utaratibu wa adhabu za makosa ya papo kwa papo, kanuni ya kuweka utaratibu katika kuwatambua wafanyakazi wageni wanaofunga ndoa na wazanzibar pamoja na kanuni ya wanafunzi wa vitendo wanaojifunza katika maeneo ya Kazi.

17) Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na Benki ya CRDB imefanya tathmini ya utoaji wa mikopo kupitia Programu ya INUKA na kuonesha mafanikio makubwa ikiwemo utoaji wa fursa za ajira 75,000, ongezeko la kipato, wajasiriamali kupata

na kumudu huduma za afya, maji na umeme. Aidha, kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 imetoa mikopo yenye thamani ya TZS 7,594,464,142 kwa Programu ya INUKA. Vile vile, Wakala imekusanya jumla ya TZS.553, 454,868.02 na imeanzisha uratibu wa utoaji wa mikopo kwa kupitia programu ya 4:4:2 ambapo jumla ya wajasiriamali 17 (Vijana 8, Wanawake 7, Watu wenye Ulemavu 2 wameomba jumla ya TZS 264,000,000 Unguja na wajasiriamali 5, (Vijana 2, Wanawake 2, Watu wenye Ulemavu 1) TZS 300,000,000 Pemba.

18) Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na PDB na Kampuni ya ORYX imetoa majiko ya gesi 1,000 kwa makundi mbalimbali ya wajasiriamali wanawake yenye thamani ya TZS. 65,000,000 kwaupande wa Unguja na zoezi kama hili litaendelea kwa upande wa Pemba. Vilevile, kwa kushirikiana na Kampuni ya Cocacola pamoja na ORYX itatoa vifaa ikiwemo mitungi ya gesi, aprons, meza, viti pamoja na masanduku ya soda yenye thamani ya TZ. 145,989,000 kwa wajasiriamali 1,698 kwa Unguja na Pemba.

19) Imefanya maonesho ya kwanza ya fahari ya Zanzibar na Marashi ya Karafuu pamoja na maonesho ya kazi zinazofanywa na Taasisi za Umma na Sekta Binafsi katika kuadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

20) Imezindua na kuweka mawe ya msingi miradi mikubwa 12 ya Uwekezaji katika maadhimisho ya Sherehe za miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

21) Imeratibu utiaji saini wa mkataba wa mradi mkubwa wa ujenzi wa bandari ya abiria katika eneo la Mpigaduri kupitia utaratibu wa miradi inayoshirikisha wazawa (PPP) pamoja na kutiliana saini hati ya makubaliano (MoU) na Taasisi za kifedha (benki ya NMB na NBC) kwa ufadhili wa miradi midogo midogo ya PPP.

22) Imekamilisha matengenezo ya PPP Portal na Muongozo ambao utatumika kwa ajili ya kupakia fursa mbali mbali za miradi inayotegemewa kutekelezwa Zanzibar.

23) Imetoa jumla ya TZS. 1,196,941,000 za fidia kwa wananchi 217 waliopo katika maeneo ya uwekezaji Micheweni Pemba na TZS. 1,494,588,719.25 kwa wananchi 555 waliopo katika maeneo ya uwekezaji Fumba Unguja.

24) Imekamilisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa Kilomita 13.5 katika eneo la uwekezaji liliopo Micheweni Pemba kwa gharama ya TZS 12.93 bilioni pamoja na kupeleka huduma za maji na umeme katika eneo hilo.

25) Imeleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Afisi pamoja na kutatua changamoto zinazowakabili wananchi na wafanyakazi katika sekta ya Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa kushirikiana na Taasisi ya PDB na uratibu wa mfumo wa Sema na Rais Mwinyi

## 3.2 CHANGAMOTO

27. **Mheshimiwa Spika,** Mbali na mafanikio yaliyopatikana, Afisi inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

1) Uhaba wa wataalamu katika fani za uhandisi, madaktari, ukaguzi kazi na wakaguzi wa vikundi vya Ushirika.

2) Uhaba wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu na mikakati iliyopangwa pamoja na fedha za kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya miradi ya PPP.

3) Uhaba wa vyombo vya usafiri pamoja na uhaba wa nafasi za Ofisi.

4) Ongezeko la asilimia 34 ya mikopo ya wajasiriamali isiorejeshwa hali ambayo imepelekea kupungua kwa utoaji wa mikopo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

5) Uhaba wa mitaji kwa ajili ya utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali kulingana na maombi ya mikopo yaliyopo yenye thamani ya TZS.95 Bilioni kwa wajasiriamali 1884 (vikundi 1,410 na wawekezaji wa ndani 474) waliomba mikopo hiyo.

## 3.3 UTATUZI WA CHANGAMOTO

1) Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa kushirikiana na Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (ARKSUU) imeanza usaili wa wafanyakazi wapya 21 (Unguja 13 na Pemba 8) kati nafasi mpya 70 zilizombwa ARKSUU. Kada zilizosailiwa ni TEHAMA, Wakaguzi Kazi, Wakaguzi wa Vyama vya Ushirika, Wahandisi wa Usalama na Afya Kazini, Takwimu na Ufuatiliaji na

Tathmini.Vile vile, Afisi imepokea jumla ya wafanyakazi 25 kutoka katika Taasisi mbali mbali za Serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi katika Taasisi yetu.

2) Afisi inaratibu utafutaji wa fedha za Ndani na Nje ya nchi kupitia wadau wa maendeleo kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Afisi, mikakati na miradi ya PPP.

3) Afisi imewasilisha Serikali Kuu michoro ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na jengo la ZIPA kwa ajili ya kupatiwa fedha za ujenzi kwa kutatua changamoto ya uhaba wa nafasi za Ofisi. Aidha kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Taasisi hizo.

4) Afisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Benki ya CRDB na ZAECA imefanya vikao vya pamoja na kuweka mikakati ya kufuatilia urejeshaji wa mikopo kwa wadaiwa sugu kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Machi, 2024 ambapo jumla ya TZS. 5,405,955,550zimerejeshwa kati ya TZS. 8,500,000,000 sawa na asilimia 64 ya madeni yaliopo.

5) Ofisi ya Rais fedha na Mipango imetenga jumla ya TZS. 39.1 Bilioni kwa ajili ya kuongeza mitaji kupitia Programu ya INUKA na Mfuko wa Khalifa Fund kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Vilevile, kupitia Programu ya Pamoja jumla ya TZS.13 Bilioni zinatarajiwa kutolewa kwa ajili ya utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Aidha, Wakala imesaini mikataba ya mashirikiano na

Taasisi mbalimbali katika utoaji wa vifaa kwa lengo la kuinua kipato cha wajasiriamali Nchini.

## 4.0 MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.

28. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kupitia fungu A07 ilifanikiwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nane na Sitini na Nane, Laki Nne na Elfu Tano na Themanini na Saba (TZS.1,864,405,087) sawa na Asilimia 94.5 ya makadirio ya mwaka ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tisa Sabini, Laki Nane na Elfu Sabini na Mbili, Mia Sita na Arobaini na Sita (TZS. 1,970,872,646). Mapato hayo yametokana na ada za usajili na ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, ada ya ukaguzi wa mikataba ya ajira nje ya Nchi, Ada ya ukaguzi wa maeneo ya kazi na vibali vya kazi.

29. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia Fungu A07 kwa kipindi cha Julai – Juni, 2022-2023, ilitumia jumla ya Shilingi Bilioni Tano, Milioni Tano, Laki Tatu Na Elfu Thelathini Na Tano Na Shilingi Thelathini Na Sita (TZS.5,005,335,036) ambayo ni sawa na asilimia 65.5 ya makadirio ya Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Sita na Arubaini na Nne, Laki Saba na Elfu Sitini na Tisa, Mia Tatu na Sabini na Nane (TZS.7,644,769,378).

30. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa Kipindi cha Julai – Juni, 2022-2023 kupitia fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) ilitumia jumla ya Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Sita Sitini Na Nane, Laki Tano

Na Elfu Kumi Na Nane, Shilingi Ishirini Na Tatu Na Senti Sabini (TZS. 7,668,518,023.70) sawa na asilimia 37.85 ya makadirio ya Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Mbili Hamsini na Tisa, Elfu Sitini Mia Mbili na Ishirini na Saba (TZS.20,259,006,227).

## 4.1 MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KWA FUNGU A07 (KAZI NA UWZEZESHAJI).

31. **Mheshimiwa Spika;** Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) ilidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Saba Thelathiuni, Mia Moja Sitini na Moja Elfu (TZS. 2,730,161,000) kupitia vianzio vya ada za usajili na ukaguzi wa vyama vya ushirika, ada ya ukaguzi wa mikataba ya ajira nje ya Nchi, ada ya ukaguzi wa maeneo ya kazi na vibali vya kazi. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024, Afisi ilipangiwa kukusanya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tisa Themanini na Mbili, Laki Nane Arobainina Tatu Elfu, Mia Tatu Sabini na Sita (TZS. 1,982,843,376).Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2024, Afisi ilifanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tisa Kumi na Sita, Laki Nane Arobaini na Mbili Elfu, Mia Tisa Arubaini na Nane na Senti Themanini (TZS. 3,916,842,948.80) ambayo sawa na asilimia 198 ya makadirio kwa mwaka 2023/2024. makusanyo hayo yamevuka lengo la mwaka kufikia asilimia

143. Kuongezeka huko kumesababishwa na mabadiliko ya kiwango cha ada kutoka Dola za Kimarekani 300 kwa mwaka hadi Dola za Kimarekani 1000 kwa miaka miwili kwa vibali vya wafanyakazi wakigeni, ongezeko la Ajira za

nje na kuongezeka kwa uthibitisho wa mikataba ya Kazi. **(Kiambatanisho nambari 4a kinahusika).**

## 4.2 MUHTASARI WA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI, 2023 - MACHI, 2024. FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI).

32. **Mheshimiwa Spika;** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) ilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Nne, Milioni Mia Tisa na Sitini na Nne, Laki Mbili Kumi na Moja Elfu, Mia Mbili na Ishirini (TZS.14,964,211,220). Afisi baada ya kuzihaulisha Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Nne na Sita, Laki Saba na Elfu Kumi na Moja, Mia Mbili Ishirini (Tsh.8,406,711,220) kwenda Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati (Small and Medium Industrial Development Agency – SMIDA) kutekeleza Kazi zao za kawaida (TZS. 1,366,105,640) pamoja na Mradi wa Ujenzi wa VituoJumuishi vya Wajasiriamali (TZS.7,040,605,580). Vile vile Afisi iliingiziwa (realocation) jumla ya Shilingi Milioni Mia Sita na Sabini na Tano, Laki Tisa na Kumi na Tatu Elfu, Mia Nane na Sita (TZS.675,913,806) ili kukidhi malipo ya Mishahara. Afisi ilibakiwa na Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Mbili na Thalathini na Tatu, Laki Nne Kumi na Tatu Elfu,Mia Nane na Sita (TZS.7,233,413,806).

33. **Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Afisi ilipangiwa matumizi ya Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Nne na Moja, Laki Tatu Elfu nne, Mia Tatu Sitini na Tatu (TZS.5,401,304,363). Kati ya fedha hizo

Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tatu Kumi na Tano, Laki Saba Ishirini na Tatu Elfu, Mia nne Themanini na Tisa (TZS. 2,315,723,489) kwa ajili ya Mishahara ya kawaida, Shilingi Milioni Mia Nane, Laki Tatu Sabini na Tano Elfu, Mia tatu Ishirini na Tatu (TZS. 800,375,323) kwa ajili ya Ruzuku ya Mishahara, Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Sita Thelathini na Tano, Laki Mbili Kumi na Nne Elfu, Mia Saba Hamsini na Moja (TZS. 1,635,214,751) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, Shilingi Milioni Mia Sita Arobaini na Tisa, Laki Tisa Tisini Elfu na Mia Nane (TZS. 649,990,800) kwa matumiziya kawaida ya Ruzuku.

34. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2024, fedha zote zilizoingizwa kwa matumizi ni Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Mbili Tisini na Tatu, Laki Nne Hamsini na Sita Elfu, Mia Tisa Thalathini na Moja (TZS. 4,293,456,931) ambayo ni sawa na asilimia 79 ya utekelezaji wa Program zote kwa kipindi cha Miezi tisa. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tatu Kumi na Tano, Laki Saba Ishirini na Tatu Elfu, Mia Nne Themanini na Tisa (TZS. 2,315,723,489) ni kwa ajili ya Mishahara ya kawaida ambayo sawa na asilimia 100, Shilingi Milioni Mia Nane, Laki Tatu Sabini na Tano Elfu, Mia Tatu Ishirini na Tatu (TZS. 800,375,323) kwa ajili ya Ruzuku ya Mishahara ambayo ni sawa na asilimia 100. Aidha Shilingi Milioni Mia Sita Tisini, Mia Nne Tisini na Tisa (TZS. 690,000,499) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo sawa na asilimia 42, Shilingi Milioni Mia Nne Themanini na Saba, Laki Tatu Hamsini na Saba Elfu, Mia Sita Ishirini (TZS. 487,357,620) ziliingizwa kwa matumizi ya Ruzuku ambayo sawa na asilimia 75, hadiMachi 31, 2024 hakuna fedha iliyoingizwa kwa kutekeleza

Miradi ya Maendeleo. **Kiambatanisho nambari 4b (i naii) vinahusika.**

**35.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi ilibakiwa na jumla ya Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Mbili na Thelathini na Tatu, Laki Nne Kumi na Tatu Elfu, Mia Nane na Sita (Tsh.7,233,413,806) ambazo zilielekezwa katika kutekeleza program zake. Jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nane na Tisini na Tatu,Laki Mbili Tisini na Nane Elfu, Mia Nne na Hamsini na Saba (TZS. 1,893,298,457) kwa ajili ya kutekeleza Programu yausimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Stahakwa wote, Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nne Hamsinina Tano, Laki Mbili Hamsini Elfu, Mia Moja na Thelathini na Tisa (TZS. 2,455,255,139) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nane Themanini na Nne. Laki Nane na Elfu Sitini, Mia mbili na Kumi (TZS. 2,884,860,210) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji.

**36.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote, hadi kufikia Mwezi Machi, 2024 ilipatiwa Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu na Ishirini na Tisa, Laki Tano Hamsini na Tano Elfu na Mia Moja na Ishirini na Tatu (TZS. 1,329,555,123) na iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Themanini na Tano, Laki Saba na Elfu Sabini na Tatu na Ishirini na Tatu (TZS.1,185,773,023) sawa na asilimia 89 ya makadirio kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake.

**37.** Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi hadi kufikia Mwezi Machi, 2024 ilipatiwa Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tisa Thelathini na Tatu, Laki Moja na Elfu Kumi na Tisa na Mia Saba na Arobaini (TSh.1,933,119,740) na imeidhinishiwa matumizi ya jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne na Tatu, Laki Tisa na Elfu Arobaini na Mbili, na Mia Sita na Hamsini na Sita (TZS. 1,403,942, 656) sawa na asilimia 73 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake.

**38.** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji hadi kufikia Mwezi Machi, 2024 imepatiwa Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Thelathini na Nane, Laki Sita na Elfu Ishirini na Tisa na Mia Tano (TZS. 2,138,629,500) na imeidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Saba na Tatu, Laki Saba na Elfu Arobaini na Moja Mia mbili na Hamsini na Mbili (TSh.1,703,741,252) sawa na asilima 80 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake.

## 4.3 MUHTASARI WA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI, 2023 - MACHI, 2024. FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI).

**39.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kupitia fungu A08 ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS. 8,232,200,000 (TZS. 770,100,000 kwa ajili ya mishahara, TZS 2,887,800,000 kwa ajili ya ruzuku ya mishahara, TZS. 1,074,300,000 kwa kazi za kawaida na TZS. 3,500,000,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo). Hata hivyo, Afisi iliingiziwa ziada ya TZS. 175,152,288 kwa ajili ya mishahara, TZS. 810,000,000 kwa ajili ya ruzuku ya mishahara Pamoja na “virement” ya TZS. 9,695,346,041 kwa ajili ya kujenga miundombinu ya

Maeneo Huru ya Micheweni, Serikali iliona umuhimu wa kuongeza rasilimali fedha kwa ajili ya kukamilisha mradi huo na kuifanya bajeti kuwa TZS. 18,912,698,329.

40. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2023 - Machi, 2024 fedha za makadirio ya matumizi ni TZS. 15,597,726,214 (TZS 602,671,654 Mishahara, TZS 2,705,850,000 Ruzuku ya Mishahara, TSZ 843,840,000 Matumizi ya kawaida na 11,445,364,560 Miradi ya Maendeleo). Hadi kufukia Mwezi Machi 2024 jumla ya TZS. 13,301,761,423 zimeingizwa sawa na asilimia 85 ya Makadirio. Kati ya fedha hizo TZS. 564,123,853 zilitumika kwa Mishahara ambayo sawa na asilimia 94 ya makadirio, TZS. 2,675,423,010 zilitumika kwa ruzuku ya mishahara ambayo sawa na asilimia 99 na TZS.366,850,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo sawa na asilimia 43 ya makadirio na TZS.9,695,364,560 sawa na asilimia 74 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. **Kiambatanisho nambari 4c (i na ii) vinahusika.**

## 5.0 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.

41. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilijiwekea malengo yafuatayo: -

1) Kukuza Uwekezaji kwa kuweka mikakati ya kutangaza fursa za uwekezaji Pemba, Visiwa vidogo vidogo, Mji mkongwe, Utalii na Uchumi wa Buluu;

2) Kuimarisha ‘ZIPA One Stop Center kwa kutoa huduma za pamoja za Uwekezaji kwa ufanisi;

3) Kuimarisha miundombinu ya Uwekezaji katika Maeneo Huru ya Uwekezaji Nchini na Ardhi ya Akiba kwa Uwekezaji;

4) Kukuza na kuimarisha Uwekezaji wa Sekta Binafsi na Sekta ya Umma katika kukuza Uchumi wa nchi;

5) Kukamilisha uandaaji wa Sera na Sheria ikiwemo Sera ya Uwekezaji Zanzibar, Sera ya Maendeleo ya Ushirika, Sera ya PPP, Sera ya Local Content, Sera ya TEHAMA ya Afisi na Sera ya Ajira. Sheria ya Uwekezaji, Sheria ya Ajira, Sheria ya Maendeleo ya Ushirika, Sheria ya Kukuza Ajira Nchini;

6) Kwa kushirikiana na ZSSF kuanzisha Mafao ya Watendajiwaliopoteza ajira;

7) Kuratibu upatikanaji wa ajira za staha ndani na nje ya nchi pamoja na kukuza ujuzi wa Vijana kuweza kujiajiri na kuajirika;

8) Kuimarisha Usalama na Afya kazini kwa ununuzi wa vifaavya uchunguzi wa afya na usalama kazini, kufanya utafiti wa maradhi yanayotokana na kazi, kufanya ukaguzi nakujenga uwezo wa watendaji;

9) Kufanya tafiti mbali mbali kwa mujibu wa Agenda za Tafiti za Afisi.

10) Kuimarisha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kutoa mikopo nafuu na mitaji;

11) Kujenga miundombinu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ikiwemo Vituo vya Kulea na Kukuza Wajasiriamali na Kituo Jumuishi cha Uwezeshaji;

12) Kuimarisha ubora na masoko ya bidhaa za Wajasiriamalikwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali na biashara;
13) Kuimarisha viwanda vidogo vidogo na vya kati vya Wajasiriamali;

14) Kuleta mabadiliko na mageuzi ya Sekta ya ushirika kwa maendeleo ya jamii na kukuza Uchumi wa Nchi;
15) Kuimarisha mashirikiano baina ya Afisi na Taasisi nyengine Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;

16) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Afisi;

17) Kukuza ujuzi wa watendaji katika kutekeleza majukumu yao; na

18) Kuimarisha ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za Afisi.

42. **Mheshimiwa Spika,** Afisi inatekeleza majukumu yake kupitia Mfumo wa bajeti ya PBB na ina mafungu 2 tofauti ya matumizi ambayo ni Fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) ambalo lina Programu kuu 3 na Programu ndogo Tisa na Fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) lenye program kuu 2 na program ndogo 4. **Kiambatanisho nambari 5 kinahusika.**

43. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa malengo na program hizi umezingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 – 2025; Dira ya Maendeleo ya 2050; Mkakati wa Maendeleo wa Zanzibar 2020/2026, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030, Afrika Tuitakayo 2030, Muongozo wa Uwekezaji Zanzibar, pamoja na Mpango Mkakati wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

## 6.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI).

## 6.1 PROGRAMU KUU PA0702: USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI KAZI NA KAZI ZA STAHA KWA WOTE.

**Matokeo ya Muda Mrefu:** Kuwepo kwa sehemu za Kazi zinazokidhi viwango vya Usalama na Afya.

44. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kuu kwa mwaka wa fedha 2023/2024 iilikadiriwa kiasi cha Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nane na Tisini na Tatu, Laki Mbili na Tisini na Nane Elfu, Mia Nne na Hamsini na Saba (TZS. 1,893,298,457) mpaka kufikia mwezi Machi, 2024 imeidhinishiwa matumizi ya jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja na Themanini na Tano, Laki Saba na Sabini na Tatu Elfu na Ishirini na Tatu (TZS. TZS.1,185,773,023) (Matumizi ya kawaida TZS. 385,397,700 na mishahara TZS. 800,375,323) sawa na asilimia 89 ya utekelezaji wa program zake ndogo.

### 6.1.1 Programu ndogo: SA070201. Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha.

45. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo (SA070101) ya uratibu na Upatikanaji wa Ajira za Staha ina lengo la kuimarisha ajira za staha. Kwa kipindi cha Julai, 2023 - Machi, 2024 programu ilikadiriwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Milioni Mia Moja Themanini na Tatu, Laki Tatu na Elfu Sitini na Tano 183,365,000/= ambapo kwa kipindi hicho Programu iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi Milioni Mia Moja Thelathini na Sita, Laki Tano na Arobaini na Mia Nne136,540,400/= sawa na asilimia 74.

46. **Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo ya Uratibu na Upatikanaji wa Ajira za Staha kwa kipindi cha mwaka 2023/2024, ilipanga upatikanaji wa ajira, kukuza ujuzikwa vijana, kuimarisha mfumo wa soko la ajira, kuweka mashirikiano na wadau, kutoa elimu na kutekeleza mpango wa ajira kwa vijana. Programu hii imetekeleza yafuatayo: -

1) Imeratibu upatikanaji wa ajira rasmi za ndani kwa Unguja na Pemba ambapo jumla ya ajira 9,630 (Wanawake 3,349 na Wanaume 6,241) zimepatikana. Ajira hizo zinajumuisha kazi za hospitali Binafsi, hoteli, Kampuni za ujenzi, Kampuni za ulinzi, skuli binafsi n.k. Aidha, kwa kushirikiana na Taasisi za Uwakala Binafsi wa Ajira, Idara imeratibu upatikanaji wa ajira za nje ya nchi kwa Vijana 3,078 (Wanaume 352 na Wanawake 2,726). Ajira hizo zimepatikana katika nchi za Oman, Kuwait, Qatar, Saudi-Arabia na UAE kwa kazi za vibarua, udereva, hoteli, ulinzi, uhudumu na kazi za majumbani.

2) Imeratibu maandalizi ya uandaaji wa Mfumo wa Taarifa za Soko la Ajira (LMIS) ambao utakuwa na kazi kubwa ya kutoa Taarifa na Matokeo muhimu yanayohusu Soko la Ajira pamoja na viashiria muhimu vya Soko la Ajira. Hatua kadhaa zimeshafanyika ikiwemo kufanya mawasiliano na Shirika la Kazi Duniani ambao ndio watakaowezesha uandaaji wa Mfumo huo.

3) Imetekeleza programu ya Internship ambapo hadi Vijana wahitimu wa fani ya TEHAMA wameshaanza katika maeneo mbali mbali ya kazi ikiwemo Shirika la Umeme (ZECO), TTCL, Zanlink, Africom nk.

4) Imeratibu Mikutano pamoja na Taasisi za Uwakala Binafsi wa Ajira kwa ajili ya kupeana taarifa muhimu zinazohusu utendaji wa kazi zao pamoja na kuandaa Rasimu ya Mkataba utakaotumiwa na Ofisi za Ubalozi kwa wafanyakazi wa Kazi za Majumbani.

5) Imeratibu kwa kushirikiana na Taasisi ya Hapa Kazi Recruitment zoezi la usaili kwa Vijana wenye ujuzi wa uhudumu (Waiter) ambapo zaidi ya Vijana 100 walijitokeza katika usaili huo. Baadhi ya Vijana hao tayari wameshawasili Nchini Kuwait kwa ajili ya kufanya kazi.

6) Imeratibu programu maalum ya kukuza ujuzi kwa Vijana wasio na Ajira, Elimu na Hawapo katika Mafunzo (NEET) kwa Vijana 55 kutoka Unguja na Pemba. Mafunzo haya kwa awamu hii yanatolewa na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Karume kwenye fani ya Ufundi Simu.

7) Imeratibu shughuli za Uwakala Binafsi wa Ajira ambapo imefanya ukaguzi katika kampuni mpya za Uwakala Binafsi wa Ajira ambazo ni Kemi Recruitment iliyopo Masingini na Sunrise Recruitment Agency iliyopo kwenye Jengo la Thabit Kombo Kisonge kwa ajili ya kujiridhisha mazingira ya ofisi kabla ya kutoa leseni za uendeshaji wa shughuli za uwakala. Aidha, Kampuni ya Afnaan Recruitment Agency, Island Recruitment Agency, Khafamous Group of Company, Global Manpower and Partner Agency na Dejure Agency zilifanyiwa ukaguzi kwa lengo la kuongezewa muda leseni zao.

8) Imeanzisha Dawati maalum la kushughulikia wafanyakazi wanaokwenda nje ya Nchi ili kuondoa changamoto mbali mbali zinazowakabili wakati wa kusafiri.

9) Imeratibu utiajі saini wa hati ya mashirikiano (MoU) na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) katika kusaidia utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Idara ikiwemo suala la wafanyakazi wanaokwenda nje ya Nchi.

10) Imeshiriki Mafunzo ya muda mfupi ya kuongeza ufanisikatika masuala ya uchambuzi wa Taarifa za Kazi na Ajira (Data Management and analysis) yaliyotolewa na Chuo cha Takwimu cha Afrika Mashariki kilichopo Dar es salaam.

11) Imeratibu mafunzo kwa kushirikiana na Taasisi ya COMHESWA na Taasisi za Uwakala Binafsi wa Ajira kwa wafanyakazi wanaotarajiwa kwenda nchini Oman kwa ajili ya kufanya kazi za ndani. Lengo la mafunzo hayo nikuhakikisha kuwa wafanyakazi hao wanatambua haki na wajibu wao katika kazi zao ili kuepukana na migogoro inayoweza kujitokeza kwenye maeneo yao ya kazi. Jumla ya wafanyakazi 95 wamepatiwa mafunzo hayo.

### 6.1.2 Programu Ndogo SA070202: Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini.

**47. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo (SA070102) ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini ina lengo la kuimarisha, masuala ya usalama na Afya katika sehemu za kazi. Kwa kipindi cha Julai, 2023 - Machi, 2024 programu ilikadiriwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Milioni Mia Moja Arobaini na Sita na Laki Mbili na Elfu Sabini na tano (TZS. 146,275,000) na iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi Milioni Sabini na Sita, Laki Tisa na Elfu Kumi Na Moja na Mia Tano (TZS. 76,911,500) sawa na asilimia 53.

48. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2023 - Machi, 2024 Programu ilipanga kufanya usajili na ukaguzi sehemu za kazi, kufanya uchunguzi wa maradhi ya ajali na maradhi yatokanayo na kazi, kukuza uelewa na kuwajengea uwezo watendaji. Programu hii imetekeleza yafuatayo:

1) Programu imefanya ukaguzi kwenye sehemu za kazi 111 (Unguja 68, Pemba 43) na kutoa miongozo kwa waajiri na waajiriwa juu ya umuhimu wa kuweka mazingira bora ya Usalama na Afya Kazini ili kujikinga na matukioya ajali na maradhi katika maeneo ya kazi. Aidha, ajali
10 ziliripotiwa na kufanyiwa uchunguzi zinazohusiana na masuala ya usalama na afya kazini.

2) Imefanya usajili wa sehemu za kazi 133 (Unguja 98, Pemba 35) kwa lengo la kuzitambua sehemu zilipo na shughuli zinazofanya ili ziweze kufikiwa kwa urahisi wakati wa ukaguzi wa Usalama na Afya Kazini na kufanya tathmini ya madhara yanayoweza kutokea ili kuweka mbinu za kukabiliana nayo.

3) Watendaji 12 wa Idara walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na Wakala wa Usalama na Afya Kazini (OSHA) Tanzania Bara kuhusiana na masuala ya usalama na afya kazini. Aidha, watendaji 4 walipatiwa mafunzo kwa vitendo kwa lengo la kuijengea uwezo Idara na watendaji na kuimarisha mashirikiano baina ya taasisi hizi mbili.

4) Ilishiriki mikutano miwili iliyoandaliwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO) Dar es Salaam kuhusiana na kuridhia Mikataba ya Kazi ya Kimataifa (Conventions Retification).

5) Imeandaa vifaa vya taarifa (information materials) kuhusiana na masuala ya usalama na afya kazini ikiwemo vipeperushi, mabango (brochures, posters) kwa ajili yakuelimisha waajiri, wafanyakazi na jamii kwa ujumla juuya masuala ya usalama na afya kazini.

6) Ilitoa mafunzo kwa wawakilishi 50 wa usalama na afya kazini (OSH focal persons) kutoka katika taasisi za umma na taasisi binafsi, lengo ni kueleweshwa majukumu yao kuhusiana na usalama na afya kazini wakiwa katika maeneo ya kazi.

### 6.1.3 Programu Ndogo SA070203: Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini.

49. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo (SA070103) ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini ina lengo la kuhakikisha kunakuwepo utekelezaji mzuri wa sheria za kazi katika sekta binafsi na sekta ya umma. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024, program ilikadiriwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Milioni Mia Tisa na Tisini na Tisa, Laki Tisa na Elfu Kumi na Tano, Mia Moja na Ishirini na Tatu (TZS 999,915,123), hadi kufikia mwezi Machi, 2024 iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya Shilingi Milioni Mia Tisa na Sabini na Mbili, Laki Tatu na Elfu Ishirini na Mojam Mia Moja na Ishirini na Tatu (TZS. 972,321,123), (Ruzuku TZS.171,945,800 na Ruzuku ya mishahara 800,375,323) sawa na asilimia 97.

50. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2023- Machi, 2024 programu ilipanga kufanya ukaguzi kazi, kuhakikisha

utekelezaji wa sheria za kazi, kuwapatia vibali vya kazi wa kigeni kuthibitisha mikataba, kusuluhisha migogoro ya kazi, kufanya ukaguzi wa vyama vya wafanyakazi na waajiri, kutoa elimu na kufanya ziara za kuwatoa Watoto kwenye ajira. Programu hii imetekeleza yafuatayo:

1) Programu imevuka malengo ya makusanyo kwa asilimia 256 kupitia vianzio vyake vya utoaji wa vibali vya kazi kwa wageni na uthibitishaji wa mikataba ya kazi ambapo ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni Moja, MilioniMia Tatu Hamsini na Sita, Laki Nane na Elfu Arobaini na Tatu, Mia Tatu na Sabini na Sita (TZS.1,356,843,376) na kufanikiwa kukusanya Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Nne Sabini na Tatu, Laki Moja na Elfu Sabini na Moja, Mia Nanena Themanini na Moja (TZS. 3,473,171,881).

2) Imeratibu utekelezaji wa sheria za kazi kwa kufanya ukaguzi katika maeneo yote ya kazi ili kuhakikisha utekelezaji wa sheria hizo. Jumla ya Taasisi 216(Unguja 141 na Pemba 75) zimefanyiwa ukaguzi kwa lengo la kusimamia na kulinda haki na Maslahi ya wafanyakazi katika sehemu za kazi, Taasisi zilizokaguliwa ni pamoja na Hoteli, Skuli binafsi, Kampuni za Ujenzi na Viwanda.

3) Imetoa Vibali vya Kazi ambapo jumla ya wafanyakazi wa kigeni 2771, walipatiwa vibali hivyo kama ifuatavyo; Waliopata msamaha wa Mheshimiwa Waziri 205, Waliopata msamaha wa miradi iliyosajiliwa ZIPA 147, Vibali vipya 787, Vibali vilivyoongezwa muda 1,086 na vya muda mfupi
546. Vibali hivi ni vya wafanyakazi kutoka katika Mataifa

mbali mbali zikiwemo nchi za Zambia, Ujerumani, Yemen, Poland, Sudan, Canada Marekani, Kenya n.k. Idadi kubwa

ya wafanyakazi waliopatiwa vibali hivyo ni kutoka katika sekta binafsi zikiwemo Skuli, Sehemu za Ujenzi, NGOs, Sehemu za Afya, Mahoteli pamoja na Utalii.

4) Imethibitisha Mikataba ya kazi kwa wafanyakazi wazawa 9,624 (Unguja 8,739 na Pemba 885). Lengo ni kuhakikisha masharti ya Mikataba hiyo inapaswa kutekelezwa ili kuendana na Sheria, kanuni na miongozo ya kazi iliopoNchini.

5) Imeendelea kushughulikia Migogoro ya kazi ambapo jumla ya migogoro 169 ilisajiliwa katika Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ambayo migogoro 57 tayari imesuluhishwa, 28 inaendelea kwenye usuluhishi (continue mediation), 42 inakwenda kufanyiwa maamuzi (arbitrated), 15 imefutwa kwa sababu walalamikaji wameshindwa kufuatilia (dismissed) na 27 imemalizika na kutolewa uamuzi (award).

6) Ukaguzi kazi maalum umefanyika wa kuangalia utekelezajiwa malipo ya kima kipya cha mshahara cha TSh. 347,000/- ambapo jumla ya Taasisi 46 kati ya 216 zilizokaguliwa Unguja na Pemba hazijatii agizo la ulipaji wa kima kipya chachini cha Mishahara. Afisi imechukua hatua ya kuwaelekeza utaratibu wa kufuata Sheria kwa kuwasilisha maombi yakulipa kima cha TSh. 250,000/= endapo Taasisi husika haitokuwa na uwezo wa kulipa kima hicho kipya. Hatua hiyoitapelekea Taasis hizo kukidhi sifa na vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria vya kutambulika kuwa ni Taasisi ndogo, vyenginevyo hatua stahiki za sheria dhidi ya Taasisi hizo zitachukuliwa ili kuhakikisha zinalipa kima husika.

7) Elimu Kazi imetolewa katika maeneo ya kazi kwa kuwapa uelewa Waajiri na Wafanyakazi juu ya taratibu za Sheria, Kanuni, miongozo na haki na wajibu katika Taasisi 30 pamoja na kurushwa hewani Vipindi 60 kwa kupitia vyombo vya habari mbalimbali vikiwemo Habari FM, Kati FM, Radio Tibirinzi, ZBC Radio na Furaha FM kwa lengo la kuwepo uhusiano bora pahala pa kazi. Aidha, elimu hiyo imejikita katika mazingira na vigezo vinavyohitajika katika kufunga Mikataba ya Kazi, masuala ya Viwango vya Ajira, njia na utaratibu wa usuluhishi na utatuzi wa migogoro katika sehemu ya kazi pamoja na athari za ajira kwa watoto.

8) Ukaguzi na uhakiki wa wafanyakazi waliopoteza ajira umefanyika kwa kuhakiki taarifa za wafanyakazi waliopoteza ajira na walioomba kulipwa fao la upotevu wa ajira, ambapo jumla ya wafanyakazi 270 waliwasilisha maombi hayo. Wafanyakazi 242 wamethibitishiwa taarifazao na kuwasilishwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) ili kuendelea na hatua nyengine na Wafanyakazi 28 maombi yao hayakuthibitishwa kutokana kwa kutowasilisha vielelezo na kutokidhi vigezo vinavyohitajika kwa mujibuwa taratibu za sheria.

9) Imeendelea usimamia uandaaji wa kanuni ambapo jumla ya kanuni tatu mpya za kazi zimekamilika zinazoweka utaratibu maalum ikiwa ni pamoja na wanafunzi kupewa kazi kwa vitendo wanaojifunza katika maeneo ya kazi (Trainees, Intern and Apprentice), Kanuni ya kuanzisha utaratibu wa adhabu za papo kwa papo (Compound offence) kwa makosa ya kutokutekelezwa kwa taratibu za sheria za kazi, pamoja na Kanuni ya kuweka utaratibu

katika kuwatambua wafanyakazi wageni wanaofunga ndoa na Wazanzibari, Kanuni hizo zilitangazwa katika gazeti rasmi la Serikali la tarehe 27 Oktoba, 2023.

10) Kwa kushirikiana na Chama cha Walimu (ZATU), Afisi ya Mrajis wa Vyama vya Wafanyakazi na Jumuiya ya Waajiri, imekamilisha mchakato wa kuipitia na kuifanyia marekebisho Katiba ya ZATU ya mwaka 2002 na tayari imeshasajiliwa kwa toleo la mwaka 2023. Imesajili Chamakipya cha Waajiri kinachohusika na sekta za Ulinzi - Private Security Employers Association (ZPSEA). Aidha, imefanya kikao cha pamoja na Vyama vyote vya Wafanyakazi kwa lengo la kujadili utendaji kazi wa vyama pamoja na changamoto zinazowakabili ili kuzitafutia ufumbuzi. Mkutano wa Utatu baina ya Serikali (Kamisheni ya kazi), Wafanyakazi (Shirikisho la vyama vya wafanyakazi – ZATUC) na Waajiri (Jumuiya ya Waajiri Zanzibar (ZANEMA), umefanyika kwa la lengo la kujadili changamoto za kazi na ajira katika kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi ili kuweka mikakati ya kuzitatua.

11) Ofisi imepokea lalamiko la ada kwa chama cha TUICO-Z Union Property na imegunduliwa kuwa mwajiri hakua akikata ada kwa vile wafanyakazi kwa madai ya kuwa wao sio wanachama wa TUICO-Z, hata hivyo, imekishauri chama hicho kufanya kikao na wafanyakazi ili kutatua lalamiko hilo.

12) Imeshiriki Mkutano wa kuandaa ripoti ya Nchi (URT) juu ya utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Shirika la Kazi Duniani (ILO), kufuatia maswali yaliyowasilishwa kwa upande wa SMT na SMZ katika utekelezaji huo. Ripoti kamili

inayowasilishwa (ILO) ni katika maeneo ya kuelewa taarifa za ukaguzi kazi, umri wa chini na kazi za kutumikishwa kwa upande wa Tanzania bara, na kukomesha kazi ya kulazimishwa na kuziainisha ajira mbaya za watoto kwa upande wa Zanzibar. Aidha, imeratibu mchakato wa kuridhia mikataba 6 ya Shirika la Kazi Duniani kwa kushirikiana na SMT na Shirika la Kazi Duniani.

## 6.2 PROGRAMU KUU PA0703: UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI.

**Matokeo ya muda mrefu:** Kila Mzanzibari anafanya Shughuliza Kiuchumi za Kumuwezesha Kumudu Mahitaji yake ya Msingi.

51. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii Kuu kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ilikadiriwa kiasi cha Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nne na Hamsini na Tano, Laki Mbilina Elfu Hamsini na Tano, Mia Moja na Thelathini na Tisa (TZS. 2,455,255,139). Mpaka kufikia mwezi Machi, 2024 iliidhinishiwa matumizi ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne na Tatu, Laki Tisa na Elfu Arobaini na Mbili, Mia Sita Hamsini na Sita (TZS. 1,403,942,656) (Matumizi ya kawaida 434,259,417 Na mishahara 969,683,239) sawa na asilimia 73 ya utekelezaji wa program zake ndogo.

### 6.2.1 Programu Ndogo: SA070301: Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

52. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo (SA070301) ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ina lengo la kuwawezesha wananchi kupata mitaji na mikopo nafuu ya kufanya shughuli za uzalishaji ili kujiajiri na kuinua

kipato chao. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Programu ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia Sita Thelathini na Saba, Mia Sita na Nne, Mia Tatu na Tano (TZS. 637,604,305/-), hadi kufikia mwezi Machi, 2024 imepatiwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Milioni Mia Sita Kumi na Nane, Laki Saba Hamsini na Tatu elfu, Mia Mbili na Ishirini na Tano (TZS 618,753,225/-) kwa matumizi ya kawaida ambapo ni sawa na asilimia 97.

53. **Mheshimiwa Spika,** Programu kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ilipanga kutoa mikopo na kusimamia marejesho ya mikopo, kuwaunganisha wajasiriamali na taasisi za fedha, kuimarisha uwezo wa wafanyakazi, kuimarisha uwekaji na usimamizi wa uwekaji wa kumbukumbu za wateja. Programu hii imetekeleza yafuatayo: -

1) Imekusanya fedha Jumla ya Shilingi Milioni Mia Tano Hamsini na Tatu Laki Nne Hamsini na Nne Elfu, Mia Nane Sitini na Nane na Senti Mbili (TZS. 553,454,868.02) zikiwa ni asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya Mikopo ya Makundi Maalum ya Wajasiriamali (wanawake, vijana na watu wenye ulemavu - 4.4.2). Programu hii imeanza ukusanyaji wa fedha hizo kuanzia mwezi wa Mei, 2022 ambapo jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Mia Moja na Sitini na Nane Milioni, Laki Tisa Hamsini na Sita Elfu, Mia Mbili Sabini na Moja na Senti Tisini na Nane (TZS. 2,168,956,271.98) zimeshakusanywa. **Rejea Kiambatanisho Nambari 2a(iii).**

   Aidha, imefanya Mikutano mitano (5) ya Masheha kwa Wilaya tano (Wilaya ya Mjini, Kusini, Kati, Wilaya ya

Kaskazini ‘A’ na Wilaya ya Kaskazini ‘B’) kwa ajili ya kuutambulisha mfuko mpya wa makundi maalum ya wajasiriamali 4.4.2 pamoja na kuwakumbushia juu ya jukumu lao kuu la kuthibitisha y za maombi ya mikopo kwa wakaazi wa shehia zao pamoja na kufuatilia shughuli walizoombea mikopo yao.

Hadi sasa jumla ya maombi 17 yamepokelewa kwa upande wa Unguja (Mjini 5, Kusini 8 na Kati 4). Na kwa upande wa Pemba, jumla ya maombi 20 yamepokelewa (Chake Chake 5, Mkoani 15). Maombi hayo yapo katika hatua ya kutathminiwa ili kupatiwa mikopo hiyo kwa mujibu wa Muongozo wa Mfuko huo (Business Model).

2) Imefanya vikao vya kamati 11 (kimoja kutoka kila Halmashauri/Manispaa) za utekelezaji wa mikopo ya makundi maalum ya wajasiriamali (4.4.2) kwa mamlaka zote za Serikali za mitaa (7 Unguja na 4 Pemba) kwa lengo la kuzipitisha kamati hizo kwenye muongozo wa mfuko huo wa Makundi Maalum ya Wajasiriamali (4:4:2) na kupeana majukumu ya kamati hizo ambayo ni kuunda vikundi vya makundi maalum, kuchambua miradi yao, kuwajazisha fomu za maombi ya mikopo kwa wale wenye sifa ya kukopeshwa pamoja na kufuatilia maendeleo ya miradi hiyo ikiwemo na urejeshaji wa fedha hizo za mikopo. Aidha, Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imekutana na Madiwani wa Manispaa ya Mjini, Baraza la Mji Kaskazini ‘B’ na Baraza la Mji Kaskazini “B” kwa lengo la kuwapa uwelewa juu ya taratibu za utoaji wa mkopo wa Makundi Maalum ya Wajasiriamali (4:4:2).

3) Imetoa mikopo kupitia programu ya Inuka yenye jumla ya TZS Bilioni Saba, Milioni Mia Tisa na Hamsini, Laki Tisa na Sitini na Nne Elfu, Mia Moja na Arobaini na Moja na Senti Themanini na Nane (TZS. 7,950,964,141.88). Mikopo hiyo imeweza kunufaisha wananchi 2,045. **Rejea Kiambatanisho nambari 2a(i).**

4) Imetoa mikopo ya vifaa vya ufugaji wa nyuki vyenye thamani ya TZS. 29,960,000 kwa vikundi ishirini na tano (25) ambavyo wamepatiwa mafunzo na kukaguliwa.

5) Imekusanya marejesho ya mikopo Jumla ya TZS. 5,405,955,550 kwa kupitia Programu mbali mbali za Mikopo **Rejea Kiambatanisho Nambari 2a (ii).**

6) Imefanya ziara (kwa upande wa Pemba) kwa vikundi 20 vyenye wanachama 161 (Wanawake 108 na Wanaume 53) kutoka Wilaya ya Mkoani kwa lengo la ufuatiliaji wa mikopo chechefu. Katika ziara hiyo, wadaiwa kutoka vikundi vitatu (3) vililipa na vilivyobakia viliweka ahadi, athari yake imeonekana takribani vikundi 12 vimefanya marejesho. Aidha, imefanya vikao na wadaiwa sugu 110 (Wanawake 21 na Wanaume 89) kutoka Wilaya zote za Pemba, baadhi ya wajasiriamali walifanya malipo na wengine walijaza hati za ahadi ya malipo.

7) Pia kwa upande wa Pemba imetoa mafunzo kwa watendaji ya kufanya tathmini ya maombi ya mikopo kupitia (tool) maalumu “Loan appraisal tools” ili kuongeza ufanisi katikakutathmini maombi ya mikopo kwa Programu Mpya (Mfukowa Makundi Malalumu 4.4.2)

### 6.2.2 Programu Ndogo: SA070302: Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika.

**54. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kusimamia Mageuzi ya Mfumo wa Vyama vya Ushirika ili viwe imara, endelevu, vinavyoendeshwa kiujasiriamali na vinavyokidhi mahitaji ya wanachama, kiuchumi na kijamii. Pia, inachangia kukuza ajira na pato la Taifa. Programu kwa kipindi cha Julai, 2023 - Machi, 2024 programu ilikadiriwa matumizi kiasi cha Shilingi Milioni Mia Sita Sitini na Mbili, Laki Tano na Elfu Ishirini na Tatu na Kumi (TZS. 662,523,010) ambapo kwa kipindi hicho Programu iliingiziwa kiasi cha Shilingi Milioni Mia Nne, Laki Moja na Elfu Ishirini na Nne, Mia Tatu na Sabini na Moja (TZS. 400,124,371) (Matumizi ya kawaida 100,696,362 na mishahara 299,428,009) sawa na asilimia 60.

**55. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2023 - Machi, 2024 Programu imepangiwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja Na Kumi na Tano na Laki Tano (TZS. 115,500,000) kutokana na Ada za Usajili na Ukaguzi kwa Vyama vya Ushirika na imefanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Arobaini na Mbili na Tisini na Nane Elfu Mia Saba na Sitini na Saba (TZS. 42,098,767) sawa na asilimia37 ya makadirio iliyojiwekea.

**56. Mheshimiwa Spika,** program kwa kipindi cha Julai, 2023 – Machi, 2024 ilipanga kusajili na kufanya ukaguzi na kutoa mafunzo kwa vyama vya ushirika. Programu hii ilitekeleza yafuatayo;

1) Imesajili vyama vya ushirika 1,645 (Unguja 791; Pemba 854), kati ya hivyo, SACCOS ni 3 na vyama vya uzalishaji na

utoaji huduma ni 1,642. Vyama vya uzalishaji vinajumuisha kilimo mchanganyiko, huduma za maduka na biashara ndogo ndogo, ufugaji, uvuvi na kazi za mikono kama vile kupamba, uchoraji, uchongaji, kudarizi, fundi gereji nk. Zoezi hili limeongeza idadi ya vyama vilivyosajiliwa kufikia5,713 (Unguja 2,805; Pemba 2,926).

2) Imekagua hesabu za Vyama vya Ushirika 354 (Unguja 116 na Pemba 238). Matokeo yameonesha vina uhaba wa elimu juu ya uendeshaji na usimamizi wa vyama. Baadhi ya vyama vinaendeshwa bila ya bajeti, mpango kazi na utunzaji usioridhisha wa kumbukumbu za hesabu na vikao. Programu inaendelea kutoa elimu, mafunzo na ushauri juu ya mapungufu yanayojitokeza. Aidha jumla ya SACCOS 4 zimekata leseni kwa kipindi hiki ambazo ni BoT SACCOS, Bandari Taxi SACCOS, Mamlaka SACCOS naAmani SACCOS.

3) Imefanya ukaguzi wa kawaida na ufuatiliaji kwa vyama 376 (Pemba 285; Unguja 91). Lengo ni kujiridhisha juu ya uendeshaji wa shughuli za vyama kwa ujumla, ikiwemo utunzaji wa vitabu vya hesabu, kumbukumbu, uendeshaji vikao n.k, zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria Nam 15 ya mwaka 2018, kanuni na sheria zao ndogondogo, pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa changamoto zinazoonekana.

4) Imetoa mafunzo mbali mbali ikiwemo ya Dhana ya Ushirika, misingi na kanuni zake, Majukumu ya Viongozi, Uhamasishaji wa mitaji kupitia SACCOS na ujazaji wa fomu za maombi ya mikopo. Jumla ya washiriki 9,706

(Wanawake 6,566; Wanaume 3,140) kutoka vyama 1,387 (Unguja; 483: Pemba 904) walipatiwa mafunzo hayo.

*5)* Kwa kushirikiana na wadau, imeadhimisha siku ya ushirika Duniani ambapo kilele cha maadhimisho hayo kilifanyika tarehe 8/7/2023 Ukumbi wa Polisi Ziwani. Washiriki walikua 414 (Wanawake 224; Wanaume 190). Maadhimisho hayo yaliambatana na shughuli za kufanya usafi, uchangiaji damu salama pamoja na Kongamano lililowashirikisha wataalamu waliobobea kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Shirikisho la SACCOS Afrika (ACOSCCA) na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC). Kauli mbiu ilikua *"Ushirika ni Wadau wa Kuharakisha Maendeleo Endelevu".*

6) Imeviunganisha vyama vya ushirika 269 (Unguja 252 na Pemba 17) kwenye taasisi za fedha ambazo ni CRDB 165, PBZ 60, Azania 29 na Equity 15 na kuwawezesha kufungua Hesabu zao katika Benki hizo. Lengo ni kurahisisha upatikanaji wa mikopo pamoja na kuwa na usalama wa kuhifadhi fedha za wanachama.

7) Imesimamia Mikutano Mikuu ya vyama vikubwa 27 vilivyofanya Mikutano iliyoambatana na chaguzi za viongozi. Lengo ni kutoa haki kwa wanachama kujadili shughuli za vyama vyao ikiwemo mafanikio na changamoto. Pia, kuidhinisha Mipango kazi na Bajeti, kujadili utekelezaji wa shughuli za ushirika, kuthibitisha wanachama wapya na kuwatoa wanachama waliokosa sifa za kuwa wanachama na kuchagua Viongozi wapya wa vyama ya ushirika. Jumla ya washiriki katika mikutano hiyo ni 1,574 (Wanawake 907: Wanaume 667).

8) Imeshiriki kutatua migogoro 6 kutoka vyama 6 vya ushirika iliyojitokeza kwa kipindi hicho, vyama vyenyewe ni Bandari Taxi SACCOS, Twitange Cooperative, Jiti jeupe coop, Jitihada Njema, Fadhila Cooperative na Vinamba Cooperative. Vyanzo vya Migogoro hiyo ni ukiukwaji wa misingi, kanuni na sheria ndogo ndogo za vyama vyao. Hatua za kuwaita wahusika na Viongozi wao kujadiliana na kufikia makubaliano, pia kuwawajibisha waliohusika na upotevu, kusimamia mgao kwa wanachama zilifanyika pamoja na kurejesha deni la mwanachama alilokopeshakwa lengo la kukarabati boti ya ushirika.

9) Imeshiriki kufanikisha maonesho ya Wajasiriamali katika Sherehe za Kizimkazi Day. Jumla ya vyama 12 vilishiriki Maonesho hayo wakiwa na bidhaa mbali mbali zikiwemo, Usarifu wa Tungule, Usarifu wa mwani, Kazi za mikono, Kutengeneza bidhaa za usumba, mikoba na vipochi, mkaa wa makaratasi, sabuni za maji, majani ya chai na ushoni. Lengo ni kutafuta masoko kwa bidhaa za wajasiriamali hao.

### 6.2.3 Programu ndogo SA070303: Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

57. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo (SA070303) ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inatekelezwa na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA) na ina lengo la kuwawezesha Wananchi katika maeneo ya mafunzo ya Ujasiriamali, uborawa bidhaa na upatikanaji wa Masoko ya uhakika na ina jukumu kuu la kubuni na kuratibu Programu za Uwezeshaji wananchi kiuchumi hasa katika maeneo hayo. Programu

hii hadi sasa inasimamia vituo vinne (4) vya mafunzo, ambavyo ni; Kituo cha kulea na kukuza Wajasiriamali kilichopo Mbweni (ZTBI), Kituo cha wanawake cha kutengeneza vifaa nya umeme wa jua kilicopo Kinyasini na vituo viwili vya usarifu wa asali kimoja kipo Kizimbani - Unguja na kimoja kipo Pujini - Pemba.

58. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024 Programu hii ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Milioni mia nne sabini na tisa laki tano thalathini elfu mia tano (TZS.479,530,500), hadi kufikia mwezi Machi, 2024 imeidhinishiwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia tatu thalathini laki tatu elfu nane mia moja thamanini na moja (TZS.330,308,181) kwa matumizi ya kawaida na mishahara sawa na asilimia 52.

59. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ilipanga kutoa mafunzo kwa wajasiriamali, kuwaunganisha na taasisi za viwango Pamoja na fursa za masoko. Programu hii imetekeleza yafuatayo: -

1) Kupitia Kituo cha kulea na kukuza wajasiriamali (ZTBI) imetoa mafunzo kwa Wajasiriamali 129 (wanaume 32 na wanawake 97) katika fani za usarifu wa mboga mboga na matunda, uokaji, utumiaji wa mashine za usarifu, uboreshaji wa bidhaa katika vifungashio na utumiaji wa mitandao katika kutangaza bidhaa.

2) Kupitia kituo cha wanawake cha kutengeza vifaa vya umeme imetoa mafunzo kwa wajasiriamali 123 (Wanaume43 na Wanawake 80) katika maeneo ya sheria na kanuni zinazohusiana na shughuli za ujasiriamali, sera ya maendeleo

ya vijana na uhifadhi wa mazingira kupitia shughuli za ujasiriamali.

3) Kupitia kituo cha Kizimbani, imetoa mafunzo ya ufugaji wa nyuki kwa wajasiriamali 38 (Wanaume 25 na Wanawake 13) wanajishughulisha na ufugaji wa nyuki.

4) Pia, Programu imetoa mafunzo kwa wananchi 1,673 (Wanaume 112 na Wanawake 1,561) kwa Unguja katika maeneo ya ufugaji wa nyuki, nadharia ya Ujasiriamali, lishe, jinsia, upatikanaji wa masoko, utunzaji wa kumbukumbu na fursa za uwezeshaji zinazopatikana katika Taasisi. Aidha, wananchi 2,016 (wanaume 321 na wanawake 1,695) kwa upande wa Pemba katika fani za uwekaji wa kumbukumbu, ujasiriamali, ushauri wa kibiashara na upatikanaji wa mikopo na matumizi yake kulingana na mradi unaotekelezwa. Pia imetengeneza zana maalum ya kukusanyia taarifa kwa ajili ya kufanya zoezi la tathmini ya mahitaji ya mafunzo kwa wajasiriamali. Lengo ni kupata taarifa kamili ambayo itaonesha aina ya mafunzo yanayohitajiwa na itasaidia uendeshaji wa mafunzo kwa mujibu wa mahitaji.

5) Imetoa mafunzo ya wakufunzi (ToT) ya Masoko ya Kidijitali (usalama wa mitandao, acount za kibiashara mtandaoni, njia za masoko ya kimtandao) kwa watendaji 23, (wanawake 13 na wanaume 10) kwa upande wa Unguja. Na kwa upande wa Pemba watendaji 25, wanawake 9 na wanaume 16 kutoka taasisi mbali mbali. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wakufunzi hao kuweza kutowa mafunzo kwa wajasiriamali, kuhusu masoko ya kidijitali na fursa mbali mbali zinazopatikana katika mtandao ili kukuza masoko ya bidhaa zao na kukuza biashara zao na kuweza kujiinua kiuchumi.

6) Kwa kuzingatia watu wenye ulemavu katika masuala ya uwezeshaji, imetoa mafunzo kwa watendaji 22 (wanawake 11, wanaume 11) kutoka Idara ya watu wenye ulemavu juu ya fursa za uwezeshaji zinazopatikana ili kuwapa uwelewawatu wenye ulemavu katika jamii.

7) Imefanya ziara kwa ajili ya kuimarisha huduma kwa kuona/ kujua changamoto na fursa zinazopatikana. Ziara hizo ni;

8) Ziara ya kuwatembelea watoa huduma za ushauri wa kibiashara (BDSPs) wakiwemo; AZSEE na ZNCC. Aidha ilishiriki katika kikao cha Pre-JCC (Joint Cordination) cha mradi wa Kaizen kwa upande wa Zanzibar, ambapo ZEEA ni mmoja wa wajumbe wa Zanzibar Kaizen Unit (ZKU) - Kitengo maalum kilichoundwa kwa upande wa Zanzibar kushughulikia mradi wa Kaizen/BDS. Aidha utayarishaji wa miongozo ya kufundishia inaendelea kutayarishwa kupitia njia ya mtandao ambapo muongozo huo ukikamilika utatumika kuwafundishia watoa huduma za ushauri kwawajasiriamali kupitia mradi wa Kaizen.

9) Ziara kwa kikundi cha watu wenye Ulemavu cha "Zanzibar Disable Bekary Assossiation" kilichopo Kwa Mchina. Ziara hiyo imebaini kuwa wajasiriamali hao pamoja na kupatamafunzo ya uokaji wa mikate mbali mbali lakini bado wanahitaji mafunzo ya ujasiriamali ili kuweza kuendeleleza biashara zao katika maeneo yao. Wakala wa UwezeshajiWananchi Kiuchumi inapanga kuwapatia mafunzo hayo katika robo mwaka ya 4.

10) Ziara kwa vikundi 45 vya ufugaji wa nyuki kwa lengo la kujua mahitaji ya vifaa, maendeleo na changamoto

zinazowakabili. Katika ziara hizo imeonekana kuwa baadhi ya vikundi vimeweza kutega mizinga, lakini hawajaweza kuvuna asali kutokana na changamoto ya uwepo wa wadudu. Hatua zilizochukuliwa ni kupatiwa ushauri wa kitaalamu kwa vikundi vilivyo na changamoto na kupatiwavifaa kwa vikundi vyenye mahitaji.

11) Ziara ya kuvitembelea vikundi 3 vinavyofanya shughuli za usarifu wa mazao, bekari na viungo vya Wilaya ya Magharibi "B". Kati ya vikundi hivyo kimoja ni kikundi cha walemavu. Ziara imebaini mafanikio na changamoto zao pamoja na kuwasaidia kuzitatua na kuwapatia ushauri wa kibiashara.

12) Ziara ya kumtembelea kijana mfugaji mbunifu katika eneo la Shakani ambae anajishughulisha na ufugaji wa kuku kwa kutumia mabanda ya kisasa kwa njia ya "cages".

13) Ziara kwa wakulima wa mananasi wa kijiji cha Donge na kufanya mazungumzo nao juu ya kusarifu mananasi. Katika mazungumzo hayo wakulima hao waliona haja ya kupatiwa mikopo na mafunzo ili kuanzisha viwanda vidogo vodogo vya kutengeneza juice na jam. ZEEA imelichukua ombi lao kwa ajili ya kulifanyia kazi. Mazungumzo hayo yaliwashirikishawakulima 14 ambao wote ni wanaume.

14) Ziara ya kwa Kampuni mbili (2) ambazo ni; Harmos bekary iliopo Mpendae na Island Diary ya Mombasa zilizonufaika na mafunzo ya ujasiriamali ili kuona matokeo ya mafunzo Ziara hiyo iligundua kuwa Kampuni ya Harmos bekary imeweza kuajiri jumla la wajasiriamali 25 na kampuni ya diary imeweza kuajiri wajasiriamali 7.

15) Kwa upande wa Pemba ilifanya ziara na mikutano na vikundi 299 kwa malengo ya kujua mafunzo yanayohitajika kuona maendeleo yao, changamoto zinazowakabili na kutoa ushauri wa kibiashara. Pia ilikutana na vikundi 27 kwa lengo la ufuatiliaji mradi wa ufugaji wa nyuki na kujua changamoto zao na kuzipatia ufumbuzi. Vikundi vyote vilipatiwa ushauri kuhusu shughuli zao. Aidha, alitembelewa Mjasiriamali mbunifu alietengeneza boti kwa kutumia plastiki, shehia ya Mwambe kwa Mtaa wa Sanani kwa lengo la kuangalia ubunifu wake na kumpa ushauri pamoja na kumuunganisha na fursa mbalimbali za Kiuchumi.

16) Kwa upande wa Pemba, jumla ya wajasiriamali 214 (wanaume 81 na wanawake 133) wamefanyiwa warsha ya uibuaji wa miradi/shughuli za kiuchumi katika maeneo yao ili kuimarisha uzalishaji na kuweza kukukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato.

17) Imefanya Tamasha la siku tatu lililopewa jina la "Fahari ya Zanzibar". Aidha lilikuwa na kauli mbiu isemayo; *"Tuwawezeshe Waajasiriamali, tuzalishe Ajira kwa kuimarisha Uchumi endelevu wa Zanzibar".* Tamasha hilo lilikuwa na lengo la kuitangaza ZEEA na fursa zinazotolewa, pia kuhamasisha wananchi kuweza kutumia bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi. Jumla ya washiriki 350 wameweza kushiriki katika Tamasha hili. Katika Tamasha hilo, matukio tofauti yalifanyika, yakiwemo; Uwasilishwaji wa mada kutoka ZEEA, Uendeshaji wa Makongamano, Utiaji wa saini Makubaliano (MoU) ya mashirikiano na Uwepo wa Maonesho ya bidhaa za Wajasiriamali zikiwemo vifaa vya ujenzi, vipodozi, viungo na mapambo ya nyumba. Tamasha

hilo limeleta mafanikio mengi yakiwemo; kuimarisha mashirikiano baina ya ZEEA na Taasisi nyengine za Serikali na zisizo za kiserikali katika masuala ya uwezeshaji, kujua fursa zinazopatikana katika Taasisi nyengine na kuwasaidia wajasiriamali kuwaunganisha na masoko.

18) Kwa upande wa Pemba, imefanya Maonesho ya Marashi ya Karafuu ya siku tatu katika viwanja vya Gombani Mpya(Korea) Wilaya ya Chake Chake Mkoa wa Kusini Pemba. Maonesho ya Marashi ya Karafuu yalifanyika kwa lengo la kuimarisha soko la ndani kwa bidhaa za wajasiriamali Pemba. Vikundi 36 vya wajasiriamali vilishiriki Maoneshohayo.

19) Kwa kushirikiana na Taasisi ya Viwango ZBS, imefanya ushajihijshaji kwa Wajasiriamali kujiorodhesha na kusajili biashara zao ili kuweza kupata alama ya ubora. Hadi sasa wajasiriamali 12 (Wanawake 8 na Wanaume 4) kwa upande wa Unguja wameshafanyiwa ukaguzi na tathmini na kwa ajili ya kupatiwa alama za ubora wa bidhaa zao. Aidha, kwa upande wa Pemba imetembelea vikundi 25 vyenye jumla ya wajasiriamali 266 (Wanawake 149, Wanaume 447) kwa lengo la kuhamasisha uzalishaji wa bidhaa zenye viwango kwa Wilaya zote za Pemba.

20) Imesaidia Wajasiriamali 194 na kampuni 8 kuwaunganisha na fursa za Masoko kupitia maonesho mbali mbali.

21) Imeratibu shindano la bidhaa za wajasirimali wanawake wabunifu ambapo jumla ya wajasiriamali 44 wanawake wameweza kujitokeza kushindanisha bidhaa zao na

hatimaekupatikana washindi watano.

60. **Mheshimiwa Spika,** Pia Programu hii imeimarishautendaji wa kazi zake kwa kufanya yafuatayo:

1) Imefanya ziara za ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli za ZEEA. Ziara hizo zilihusisha wanufaika 13 wanawake wamafunzo na wanufaika 14 (wanaume 8 na wanawake 6) wa Mikopo. Ziara imebaini kwamba baadhi ya wanufaika wanachangamoto ya kushindwa kulipa kiwango cha fedha kinachotakiwa kulipwa kwa mwezi. Hata hivyo, tathmni inaonesha kuwa wanufaika hao wameweza kuzalisha ajira mpya 25 (wanaume 8 na wanawake 17). Pia ilifanya Tathmini kwa miradi 18 iliyopatiwa mikopo kupitia Khalifa Fund, tathmini hiyo ilionesha kuwa wamiliki wa miradi hiyo wanakabiliwa na baadhi ya changamoto katika shughuli zao ikiwemo kodo, hata hivyo miradi hiyo imefanikiwa kuzalisha ajira mpya 40 (wanaume 18 na wanawake 22). Aidha, kwa upande wa Pemba, imefanya tathmini ndogo ya matokeo ya mikopo ambapo imewafikia wanufaika 213 kuangalia athari za mikopo katika kukuza miradi ya uzalishaji pamoja na kusikiliza changamoto zao na kuzitatua.

2) Imeratibu vikao saba (7) vya Kamati za Bodi na viwili vya Bodi. Vikao hivyo vilijadili, kupokea na kuridhia taarifa mbali mbali zikiwemo hesabu za Mwaka wa fedha 2022/2023(Final Account), utekelezaji wa Mpangokazi, taarifa ya mapato na matumizi, taarifa na muenendo wa mikopo naMiongozo inayohitajika katika kazi za ZEEA.

3) Imewapatia mafunzo ya ndani watendaji. Mafunzo hayo yanahusu namna ya kuwasiliana kwa kutumia Barua pepe (Email). Mafunzo hayo yamesaidia katika kuimarisha mawasiliano. Aidha, kwa kushirikiana na Mamlaka ya

Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, imetoa mafunzo juu ya kukabiliana na rushwa na uhujumu uchumi. Kwa upande wa Pemba, Wafanyakazi wamepatiwa mafunzo juu ya uwajibikaji na utekelezaji wa shughuli mbalimbali ili kuongeza ufanisi na utendaji wa kazi.

4) Imeingia makubaliano (MoU) saba (7) kwa lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi.

5) Imetangaza huduma na mafanikio ya Taasisi kwa kutumia vyombo vya habari ambapo ilifanikiwa kuandaa vipindi vinane vya Redio na vipindi sita vya TV kupitia ZBC na ZCTV. Aidha, imetumia mitandao ya kijamii ikiwemo ukurasa wa Facebook, Instagram na Youtube. Aidha kushiriki katika kipindi cha Mkono kwa mkono katika Mikoa mitano na kupata fursa ya kuelezea fursa zinazopatikana na kuwezakujibu masuala ya wananchi walioshiriki.

## 6.3 PROGRAMU KUU PA0705: UENDESHAJI NA URATIBU WA OFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI.

**Matokeo ya Muda Mrefu:** Kukuza uwezo wa Afisi kutekeleza majukumu yake katika masuala ya Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

61. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii Kuu kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 ilikadiriwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja na Thelathini na Nane, Laki Sita na Elfu Ishirini na Tisa na Mia Tano (TZS. 2,138,629,500) hadi kufikia mwezi Machi, 2024 imeidhinishiwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Saba na Tatu na

Elfu Arobaini na Moja, Mia Mbili na Hamsini na Mbili (TZS. 1,703,741,252) (Matumizi ya kawaida TZS. 357,701,002 na Mishahara 1,346,040,250) sawa na asilimia 80 ya utekelezaji.

### 6.3.1 Programu ndogo SA070501: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi.

62. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo SA070501 ya uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi ina lengo la kuratibu uandaaji na utekelezaji wa Sera, Sheria, Mipango, Bajeti, Tafiti na Mashirikiano ya Afisi na Taasisi nyengine ndani na nje ya Nchi.

63. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo SA070501 ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi, kwa kipindi cha Julai, 2023 - Machi, Julai, 2024 ilikadiriwa matumizi kiasi cha Shilingi Milioni Mia Tatu na Hamsini na Nane, Laki Nne na ishirini na Mbili Elfu na Mia Nane (TZS. 358,422,800) ambapo kwa kipindi hicho Programu iliidhinishiwa kiasi chaShilingi Milioni Mia Mbili na Kumi na Nane, Laki Nane elfu Tano, Mia Tano na Hamsini (TZS. 218,805,550) (matumizi ya kawaida 69,007,000 Na mshahara 149,798,550) sawa na asilimia 61.

64. **Mheshimiwa Spika,** Programu kwa kipindi Julai, 2023 - Machi, 2024 ilipanga kufanya mapitio ya sera, kufanya tafiti, ufuatliaji na tathmini Pamoja na kuratibu mipango na miradi ya Afisi. Programu hii imetekeleza shughuli zifuatazo: -

1) Imeratibu utayarishaji wa ripoti mbalimbali za utekelezaji ikiwemo, ripoti ya utekelezaji wa Ilani ya CCM 2020/2025, Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Ripoti ya utekelezaji wa maendeleo ya Zanzibar 2021/2026, Ripoti ya ufuatiliaji wa vipaumbele vya Mheshimiwa Rais kupitia PDB na ripoti maalum zilizohitajika kwa vipindi tofauti zinazohusiana na utekelezaji wa shughuli za afisi kupitiaIdara na Taasisi mbalimbali.

2) Imeendesha mafunzo ya Takwimu kwa watendaji 60 (30 Unguja na 30 Pemba) wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kutoka Idara zote za Afisi hiyo. Mafunzo hayo yalilenga kujenga uelewa kwa watendaji wa Afisi juu ya Masuala ya Takwimu pamoja na viashiria vinavyotumika katika kukusanya Takwimu. Kufuatia mafunzo hayo, viashiria vya kukusanya takwimu kwa kila Idara vimetengenezwa.

3) Imefanya utafiti wa taarifa za Ajira katika Sekta rasmi na Sekta isiyo rasmi Zanzibar kwa lengo la kupata takwimu halisi za ajira laki tatu kufikia mwaka 2025. Utafiti huo umesaidia kutambua shughuli za kiuchumi na kijamii zinazofanyika Nchini na kutambua aina za kazi zinazofanywa na Wananchi kulingana na jinsi, jinsia na mikataba yao. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa jumla ya ajira zilizozalishwa kuanzia Novemba, 2020 hadi Septemba, 2023 ni 187,651 ambapo kati ya ajira hizo, Wanaume 93,029 (49.6%) na Wanawake 94,622 (50.4%). Kwa upande wa ajira za Serikali, jumla ya wafanyakazi 3,349 (Wanaume 1,289 (38.4%) na Wanawake 2,060 (61.6%)) wameajiriwa Serikalini katika kada mbali mbali. Jumla ya wafanyakazi 52,501 (Wanaume 20,768 (39.5%) na Wanawake 31,733 (60.5%)) wameajiriwa

katika miradi ya maendeleo, na jumla ya wafanyakazi 3,855 (Wanaume 884 (22.9%) na Wanawake 2,971(77.1%)) wamepata ajira za nje ya nchi. Kwa upande wa uraia, asilimia kubwa ya walioajiriwa ni Wazawa kutoka Zanzibar (110,829) sawa na asilimia 86.6, ikifuatiwa na wanaotoka Tanzania Bara (15,735) sawa na asilimia 12.3, na wageni (1,382) sawa na asilimia 1.1.

4) Imeandaa andiko la nadharia (concept note) juu ya uratibu, ufuatiliaji na tathmini katika Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji na andiko la nadharia la takwimu za kiutawala katika Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji. Maandiko hayo yatasaidia kuimarisha shughuli za uratibu, ufuatiliaji na tahthmini pamoja na kuimarisha masuala ya takwimu za Afisi.

5) Imefanya safari ya kikazi Pemba kushiriki ziara ya Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi, vile vile imefanya safari ya kikazi Dar es salam kushiriki kikao cha kupitia maandiko yamiradi na Benki ya Dunia.

6) Imeandaa Rasimu ya Sera ya TEHAMA ili kutoa muongozo wa masuala ya TEHAMA kwa utekelezaji wa shughuli za Afisi.

7) Imeandaa Mpango wa Utekelezaji wa Rasimu ya Sera mpya ya Ajira.

8) Imefanya Ufuatiliaji katika Kituo cha Kulea na kukuza wajasiriamali ambapo kituo hiki kilitoa mafunzo kwa wajasiriamali katika fani za ‘E – marketing’ na usarifu wa matunda na mbogamboga. Aidha, imefanya ufuatiliaji Unguja na Pemba kwa wanufaika wa Mradi wa Kuwawezesha Vijana na Wanawake katika Ufugaji wa Nyuki kwa njia ya

kisasa ili waweze kupata ajira na kuongeza kipato ambapo wanufaika hao walipatiwa mafunzo, ushauri wa kitaalamu na vifaa vya kufugia nyuki.

9) Kwa kushirikiana na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (ZEEA), programu imefanya Ufuatiliaji kwa wanufaika wa mikopo ya Mradi wa Mfuko wa Khalifa (Khalifa Fund), matokeo yameonesha asilimia 100 ya mikopo iliyotolewa imetumika katika shughuli zilizoombewa, asilimia 75 ya walionufaika na mikopo wanaendelea vizuri na shughuli zao kwa kuongeza uzalishaji kwa zaidi ya asilimia 65 Kutoka asilimia 25 za mwanzo, kuongezeka mitaji yao kwa wastani wa asilimia 55 na kuimarisha ubora wa bidhaakwa zaidi ya asilimia 87. Aidha, asilimia 90 ya wanufaika hao wamechangia katika suala la kutoa ajira kwa wananchi wakiwemo wale wanaoishi maeneo ya karibu na miradi husika kati ya watu 4 hadi 8.

Kwa ujumla takriban wanufaika wote wanafanya vizuri katika marejesho ya mikopo hiyo kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ). Pamoja na mafanikio hayo pia wanakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo: -

Ukosefu wa gredi ya Umeme wa uhakika kwa Mujibu wa uwezo wa mitambo na uzalishaji wa Viwanda, Uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya Zanzibar zinazofanana na zile zinazozalishwa Zanzibar ambazo huuzwa kwa bei rahisi sana na kuangusha soko lao na Kutozwa ushuru kwa malighafi ambazo zinakusudiwa kutumika kwa ajili ya uzalishaji wa viwanda vya ndani vya Zanzibar.

### 6.3.2 Programu ndogo SA070502: Utawala na Uendeshaji.

65. **Mheshimiwa Spika,** Programu SA070502 ya Utawala na Uendeshaji ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Uendeshaji na Utumishi na kukuza uwezo wa Taasisi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kwa kipindi cha Julai, 2023 – Machi, 2024 ilikadiriwa matumizi kiasi cha Shilingi Milioni Mia Nane na Tisini na Tatu. Laki Sita na Sabini na Sita Elfu, Mia Sita na Sabini na Mbili (TZS. 893,676,672) ambapo kwa kipindi hicho Programu iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi Milioni Mia Saba na Sitini na Nne, Sabini na Nne Elfu, Mia Mbili na Sabini na Mbili (TZS. 764,074,272) (matumizi ya kawaida TZS. 191,862,600 Na mshahara TZS. 572,211,672) sawa na asilimia 85.

66. **Mheshimiwa Spika,** Programu kwa kipindi Julai, 2023 - Machi, 2024 ilipanga kusimamia maslahi ya wafanyakazi, kufuatilia viinua mgongo, kutoa mafunzo na mpango wa rasilimali watu na ununuzi wa vifaa. Programu hii imetekeleza shughuli zifuatazo: -

1) Imesimamia malipo ya safari sitini (60) za ndani za Kikazi kwa Viongozi wa Afisi pamoja na Maafisa kwenda Pemba,Dar es salaam, Arusha na Dodoma.

2) Imefanya matengenezo ya gari sita, vespa mbili na kukatia bima gari nne ili kuweza kuleta urahisi katika kazi za kiofisi.

3) Imegharamia malipo ya umeme, magazeti, vitasa vinne vya milango na mafuta kwa ajili ya kufuatilia shughuli mbali mbali za Afisi.

4) Imelipia Gharama za mkonga wa mawasiliano kwa ajili huduma za mtandao (internet) pamoja na matengenezo ya internet katika jengo la Wizara.

5) Imeratibu kazi ya uingizaji wa msimbomilia (barcode) katika Mfumo wa Uhifadhi wa Mali za Serikali.

6) Imeratibu vikao vya bodi ya zabuni 8, vikao 2 vya Kamati ya Ukaguzi wa ndani pamoja vikao 3 vya Kamati ya Uongozi wa Wizara.

7) Imesimamia na kugharamia usaili wa wafanyakazi wapyaUnguja na Pemba.

8) Imeratibu kazi ya uingizaji wa taarifa za Wafanyakazi kwenye mfumo wa HRM- PAYROLL.

9) Imefanya malipo kwa vitu mbali mbali vikiwemo vifaa vya usafi, samani (furniture), adapter, ununuzi wa tenki la maji, matengenezo ya vifaa vya kuzimia moto (fire extinguisher), na vitabu vya hesabu (LPO) kwa ajili ya manunuzi.

10) Imefanya malipo ya ubani kwa Wafanyakazi wawili (2) waliofiwa na wazazi na malipo ya ubani kwa Mfanyakazi (1) aliyefariki.

11) Imewapatia mafunzo ya muda mfupi ya ndani ya Nchi Wafanyakazi wanne (4) (wanawake 3 na mwanamme 1), ambao wapo katika kitengo cha Habari na Sekretari (1). Aidha, Wafanyakazi watatu wamelipwa kwa ajili ya kupatiwa mafunzo ya Mfumo wa Vibali vya Nje wakiwemo Maafisa Utumishi (2) na Afisa Tehama (1). Vile vile, malipo ya mafunzo kwa wahasibu watatu (3) kwa mafunzo ya mfumowa IFMS yamefanyika.

12) Imefanya malipo ya muda wa ziada (overtime) kwa ajili ya Wafanyakazi watano ambao ni wahasibu watatu (3), Maafisa manunuzi (2) na Maafisa sita wa usimamizi wa mali za Umma wakiwemo Wanawake 3 na Wanaume 3, malipo ya posho la likizo kwa Wafanyakazi tisa na malipo ya malimbikizo ya mshahara kwa Wafanyakazi watatu.

### 6.3.3 Programu ndogo SA070503: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba.

67. **Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo ya uratibu na utekelezaji wa shughuli za Afisi Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Afisi Pemba ambayo inahusisha Idara ya Uendeshaji na Utumishi pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Programu ndogo kwa kipindi cha Julai, 2023 - Machi, 2024 ilikadiriwa matumizi kiasi cha Shilingi Milioni Mia Nane na Themanini na Sita, Laki Tano na Thelathini Elfu na Ishirini na Nane (TZS. 886,530,028) hadi kufikia mwezi Machi, 2024, Programu imeingiziwa Shilingi Bilioni Mia Saba na Ishirini, Laki Nane na Sitini na Moja Elfu, Mia Tano na Kumi na Nane (TZS. 720,861,518) (Matumizi ya kawaida TZS. 96,831,402 na mishahara TZS. 624,030,028) sawa na asilimia 81 ya makadirio.

68. **Mheshimiwa Spika,** Programu kwa kipindi cha Julai, 2023 – Machi, 2024 ilipanga kusimamia utekelezaji wa Sera sheria na miongozo, kutoa mafunzo ya muda mref na ufupi, kufanya utafiti, kuandaa taarifa za utekelzaji na kutoa vipindi. Programu hii imetekeleza yafuatayo:

1) Imesimamia vyema maslahi ya wafanyakazi kwa kulipa fedha za likizo kwa watendaji Ishirini (20) (Wanawake 12 na Wanaume 8) na kulipa posho la masaa ya ziada kwa wafanyakazi wanne (4) Wanaume. Afisi imempatia mafunzo ya muda mrefu mfanyakazi mmoja (1) Mwanamke katika fani ya Ukatibu Mukhtasi na imewapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi Kumi na Tatu (13) Wanaume 8 na Wanawake (5)katika mafunzo ya mfumo wa Rasilimali watu na uandishi wa ripoti ya IPSAS, kompyuta na udereva. Pia, imelipia gharama za ubani kwa mfanyakazi mmoja (1) Mwanamme nakufanya malipo ya safari za ndani ya Nchi kwa ajili ya kushiriki katikavikao na shughuli mbali mbali za Afisi Unguja.

2) Imefanya manunuzi ya mafuta, viburudishaji, vifaa vya kuandikia na magazeti ya kila siku pamoja na kulipia gharama za umeme, maji, huduma za mtandaona gharama za usafi kwa kampuni inayotoa huduma ya usafi katika Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji. Pia, imelipia gharama za bima na kufanya matengenezo ya magari, AC na printa za Afisi.

3) Imeandaa makala maalum (documentary) kueleza mafanikio waliyoyapata wananchi katika kipindi cha awamu ya nane kupitia Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu na elimu ya kuendesha shughuli za kibiashara kupitia Mitandao ya Kijamii. Aidha, Afisi imeandaa na kurushwa hewani vipindi Kumi (10) kupitia Televisheni na Redio. Pia imeandaa Makala za magazeti Sita (6) na Stori Kumi (10) kueleza mafanikio ya programu za Kazi na Uwezeshaji na huduma zinazotolewa. Hadi kufikia mwezi Machi 2024, Afisi inaendelea kukamilisha Jarida la "Uwezeshaji Pemba"

ambalo litaeleza utekelezaji wa kazi za Afisi na mafanikio ya Programu ya Kazi na Uwezeshaji.

4) Imefanya ufuatiliaji na tathmini kwa madhumuni ya kuimarisha utendaji wa shughuli za Afisi na kutatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu mbali mbali. Ufuatiliaji huo ulifanyika katika Taasisi binafsi ili kuhakikisha sheria za kazi zinafuatwa kutokana ukaguzi na elimu inayotolewa na Kamisheni ya Kazi na Idara ya Usalama na Afya kazini. Taasisi zilizofanyiwa ufuatiliaji zinaendelea na kusimamia na kutekeleza sheria za kazi ipasavyo. Aidha, katika kuboresha masuala ya ufauatiliaji, Afisi imetoa mafunzo ya ndani kwa watendaji 15 (Wanawake 7 na Wanaume 8) yanayohusu ufuatiliaji na tathmini na kuandaa zana (tools) kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli mbali mbali.

5) Imeratibu maendeleo ya Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kufanya ziara katika kituo cha kuchakata asali Pujini na vikundi vya ushirika kwa wanufaika wa fedha za IMF za ahueni ya UVIKO19 kwa lengo la kuangalia mafanikio, changamoto na kuhamasisha urejeshaji wa mikopo hiyo kwa wakati. Ziara hizi zimebaini kuwa wajasiriamali wanahitaji mafunzo kulingana na sekta wanazofanyia kazi, uwekaji wa kumbukumbu na ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kusaidia kutatua changamoto zao mara tu zinapowakabili.

6) Afisi imefanya kikao kimoja cha wajumbe wa TDT (Technical Delivery Team) Pemba kwa lengo la kuandaaa mpango wa ufuatiliaji wa miradi wa sekta zinazotoa huduma za jamii Pemba. Aidha, imefanya ziara za ufuatiliaji wa madeni ya Mikopo inayotolewa na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi

Kiuchumi (ZEEA) katika shehia 5 za Wilaya ya Chake Chake

kwa Wadaiwa 77. Matokeo ya ziara hii ni asilimia 3.8% miradi ya wadaiwa haikupatikana, 9.1% Wadaiwa walianza kulipa siku ya zoezi la ufuatiliaji na 87% waliweka ahadi ya kuanza kulipa katika tarehe zinazofuata kwa maandishi.

7) Kwa kushirikiana na Afisi kuu Unguja imeratibu kikao kimoja cha siku mbili kwa watendaji wa zoezi la kukusanya Takwimu za Ajira linalosimamiwa na PDB kwa lengo la kupata takwimu sahihi zilizozalishwa kwa kipindi cha miaka 3 ya awamu ya nane. Aidha, imetoa mafunzo ya takwimu kwa watendaji 30 (Wanawake 10 na Wanaume 20) wa Afisiya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji ili kuwawezesha kuwekatakwimu vizuri kulingana na mahitaji.

8) Afisi imetoa mafunzo ya uandaaji wa ripoti mbali mbali kwa watendaji wa Afisi ili kuwasaidia watendaji kuwa na mfumo unaofanana katika uandishi wao wa ripoti kulingana na aina ya ripoti inayohitajika. Aidha, imetoa mafunzo ya Utawala Bora na Sheria ya Utumishi wa Ummakwa watendaji 37 (Wanawake 19 na Wanaume 18) kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na upatikanaji wa haki za watendaji.

9) Afisi kwa kushirikiana na Wakala wa Uwezeshaji WananchiKiuchumi imeratibu na kutoa mafunzo ya uandaaji wa miradi kwa timu ya wasimamizi wa miradi (Project Management Team). Aidha, imeandaa maandiko ya miradi inayohusu “Support Disadvantage Seacocumbers Fermers in Fundo” na “Strengthen Cooperatives Financial recilience and Climatic Adaption in Pemba” kwa ajili ya kuomba fedha kutoka kwa wadau mbali mbali wa maendeleo ili kusaidia wajasiriamali kuendesha shughuli zao kiufanisi.

10) Afisi kwa kushirikiana na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imeratibu na kufanya maonesho ya Wajasiriamali "Jukwaa la Marashi ya Karafuu" kwa lengo la kutangaza, kuuza na kutoa fursa ya kuwakutanisha wajasiriamali kuweza kubadilishana uzoefu na kujenga mtandao wa pamoja ambao utasaidia kuwaunganisha wajasiriamali na kuweza kuzijua fursa mbali mbali ambazo zinapatikana Nchini ili kuhakikisha wajasiriamali wote wa Zanzibar wanafaidika nazo.

11) Afisi kwa kushirikiana na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kampuni ya Coca cola imeratibu na kutoa mafunzo ya wajasiriamali wanawake 1,089 walioshiriki katika Proramu ya "Mwanamke shujaa". Lengo la Programu hii ni kumuwezesha mwanamke kujikwamua na umaskiniwa kipato kuweza kujiajiri.

12) Afisi kwa kushirikiana na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Ofisi ya Pemba imefanya Upembuzi yakinifu ya miradi 13 ya wajasiriamali kutoka Wilaya ya Chake Chake ambao wameomba Mikopo kupitia Programu ya 4:4:2. Katika upembuzi huo Jumla ya fomu 7 zimerejeshwa kwa kutokidhi vigezo na fomu 5 tu zimefaulu kwa uchambuzi wa awali. Baada ya kufanya ukaguzi katika maeneo ya miradiJumla ya miradi miwili (2) ndio imekidhi vigezo kwa hatuaya kupelekwa benki.

13) Imeratibu utayarishaji wa ripoti mbalimbali za utekelezaji zikiwemo, ripoti ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020–2025, ripoti zilizowasilishwa katika kamati mbali mbali za Baraza la Wawakilishi, na ripoti maalum zilizohitajika kwa vipindi tofauti zinazohusiana na utekelezajiwa shughuli za Afisi katika taasisi mbali mbali.

14) Inaendelea na kusimamia maslahi ya wafanyakazi, utoaji wa mafunzo, kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria mbalimbali, kuandaa maandiko ya miradi, tafiti, kuandaa taarifa za utekelezaji na kufanya shughuli za ufuatiliaji na tathmini za Afisi pamoja na kuripoti utekelezaji wake.

## 7.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)

## 7.1 PROGRAMU KUU: PA0801 KUIMARISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI.

**Matokeo ya muda mrefu:** Usimamizi na Ushajihishaji wa maliza umma kwa kuziweka katika mfumo wa mashirikiano kwa wote.

**69. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kuu kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ilikadiriwa kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Tano na Tisini na Saba, Laki Saba na Ishirini na Sita Elfu Mia Mbili na Kumi na Nne (TZS. 15,597,726,214). mpaka kufikia mwezi Machi, 2024 iliidhinishiwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Tatu na Moja, Laki Saba na Sitini na Moja Elfu, Mia Nne na Ishirini na Tatu (TZS. 13,301,761,423) (matumizi ya kawaida Shilingi Milioni Mia Tatu Sitini na Sita, Laki Nane Hamsini Elfu (TZS. 366,850,000) mishahara Bilioni Tatu, Milioni Mia Mbili na Thelathini na Tisa, Laki Tano na Arobaini na Sita Elfu, Mia Nane na Sitini na Tatu (TZS. 3,239,546,863) sawa na asilimia 85.28 ya utekelezajiprogramu zake ndogo.

### 7.1.1 Programu ndogo SA080101: Mashirikiano bainaya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

70. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Kuimarisha Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ina lengo la kukuza kuratibu na kuimarisha mashirikiano baina ya sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika Sekta za kiuchumi na kijamii pamoja na kutekeleza miradi mbali mbali ya maendeleo.

71. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi, 2024 Program ya Mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi ilikadiriwa jumla ya matumizi ya Shilingi Milioni Mia Tatu sitini na nne, laki mbili na elfu tatu mia nane na kumi na sita TZS. 364,203,816 (TZS 97,873,816 Mishahara, TZS 266,330,000 Matummizi ya kawaida) na imefanikiwa kuingiziwa jumla ya Shilingi Milioni Mia moja sitini na moja, themanini na moja elfu, mia saba na sitini na tano TZS. 161,081,765 (TZS 97,781,765 Mishahara na TZS. 63,300,000 Matumizi ya kawaida) ambayo ni sawa na asilimia 44.2 ya makadirio kwa kipindi hicho.

72. **Mheshimiwa Spika,** programu kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kuratibu miradi ya PPP, kusimamia utekelzaji wa miradi ya PPP, kufanya na kushiriki mijadala, kufanya ukaguzi na kujenga uwezo kwa wafanyakazi. Programu hii imetekeleza shughuli zifuatazo:

    1) Imehudhuria warsha mkoani Arusha ambayo imeandaliwa na Benki ya Dunia na kuhudhuria na Taasisi na Wizara za Serikali, lengo la warsha hii ni kupeana uelewa juu ya taratibu za uandaaji, utekelezaji

na usimamizi wa mradi.

Vile vile, kupena uelewa juu ya masuala ya kifedha na kiutendaji na kupatiwa uzoefu wa namna ya utekelezaji wa miradi ambayo Benki ya Dunia wameweza kuifadhili katika maeneo mengine duniani.

2) Imefanya ziara ya kutembelea Wizara zote za SerikaliyaMapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kufuatilia hali ya utekelezaji wa miradi ya PPP na kutambua changamotowanazopambana nazo na kuzipatia ufumbuzi. Kupitia ziarahio ilikusanya taarifa za miradi kutoka katika Mamlaka za utekelezaji kwa ajili ya kuandaa taarifa fupi za miradi ya PPP za awamu ya pili (PPP project profile bundle II).

3) Inaendelea kufanya vikao mbali mbali vinavyohusu uwekezaji wa miradi ya PPP, Vikao hivyo vilihusisha mamlaka husika za utekelezaji pamoja na wawekezaji walioonesha nia ya kuwekeza, miongoni mwa kampuni hizo ni Meva, Simba, AGL, Ecobell, Sogea Satom, ZF Devco, Xpanishna Air pay. Uwekezaji wa Miradi utafanyika mara baada ya kukamilishataratibu za uwekezaji.

4) Imefanya uchambuzi wa maeneo makuu ya makubaliano (key head of agreements) ya mradi wa ukusanyaji wa maji taka, mradi huu umewasilishwa na unategemewa kutekelezwa na kampuni ya Sogea Satom, una lengo la kukusanya maji taka katika maeneo ya Mji Mkongwe, ya kibiashara na katika hoteli za kitalii. Kwa sasa mradi huu upo katika hatua ya GNT.

5) Imefanya tathmini ya kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa ukaguzi wa vyombo vya moto (Motor Vehicle Inspection), mshauri

elekezi atakaepatikana atafanya kazi katika mradi huu hadi atakapopatika na mwekezaji.

6) Imepata mafunzo ya kuratibu portal ya Idara ya PPP, portal hii ina lengo la kuwarahisisishia wawekezaji kuona fursa za uwekezaji wa miradi ya PPP Zanzibar na kutuma maombi yao, miongoni mwa mafunzo hayo ni namna ya kupakia miradi ya PPP, kuangalia maombi yaliyotumwa na kuwajibu wawekezaji.

7) Imehudhuria vikao mbali mbali vilivyofanyika Tanzania Bara, vyenye lengo la kubadilishana mawazo namna gani miradi ya PPP inaweza kutekelezwa kwa urahisi, vikao vya wawekezaji ambavyo vinafanyika Tanzania Bara na kikao cha maandalizi ya Rasimu ya Mkataba wa Uwekezaji kati ya Nchi Mbili (BIT) chenye lengo la kukuza na kulinda uwekezaji kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Indonesia.

8) Imerusha hewani kipindi kinachohusu kutoa taaluma ya dhana ya utekelezaji wa miradi kwa njia ya Mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi kupitia televisheni ya Shirika la Utangazi Tanzania (TBC).

9) Imetiliana saini na kampuni ya ZF DEVCO kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya abiria katika eneo la Mpigaduri Maruhubi, mradi huo utatekelezwa kwa mfumo wa PPP, ujenzi wa mradi huo unategemewa kuanza karibuni.

### 7.1.2 Programu ndogo SA080102: Maendeleo ya Ukuajiwa Uchumi kupitia Uwekezaji.

73. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kushajihisha Uwekezaji ndani na Nje ya Nchi na kuweka mazingira mazuri ya kisera, kisheria ya uimarishaji wa

huduma mbali mbali zitakazoimarisha Uwekezaji Nchini. Kwa kipindi cha (Julai, 2023 - Machi, 2024) Programu ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Bilioni Kumi na mbili, milioni mia nne na moja, laki mbili na kumi na nne elfu, mia tano na sitini TZS 12,401,214,560 (TZS. 2,705,850,000 kwa ajili ya mishahara na TZS. 9,695,364,560 Miradi ya maendeleo). Hadi mwezi Machi, 2024 programu ilipatiwa matumizi ya Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Tatuna Sabini, Laki Saba na Themanini na Saba Elfu, Mia Tano na Sabini TZS. 12,370,787,570 Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Sita na Sabini na Tano, Laki Nne na Ishirini na Tatu Elfu na Kumi (TZS. 2,675,423,010) kwa ajili ya Ruzuku ya mishahara ambayo sawa na asilimia 98.9 na Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Sita na Tisini na Tano, Laki Tatu na Sitini na Nne Elfu, Mia Tano na Sitini (TZS. 9,695,364,560) ni kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleoambayo sawa na asilimia 84.71.

74. **Mheshimiwa Spika,** Programu kwa kipindi cha Julai, 2023 – Machi, 2024 ilipanga kutangaza fursa za uwekezaji na kufanya usajili wa miradi, itajenga na kuendeleza miundo mbinu, itaharakisha upatikanaji wa maeneo ya Akiba,kuunganisha mfumo wa kieloktroniki na kukamilisha sheria mpya uwekezaji. Programu hii imetekeleza yafuatayo:

1) Imekusanya Jumla ya TZS. 3,612,236,760.08 ya makadirio ya TZS 2,976,285,884.94 ambayo ni sawa na asilimia 121 ya makadirio ya Miezi Tisa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Mamlaka (ZIPA).

2) Kuendelea na jukumu lake la kuitangaza Zanzibar kwa Wawekezaji juu ya fursa za uwekezaji zilizopo nchini kwa

lengo la kuleta wawekezaji wenye mitaji mikubwa katika sekta zote za uchumi wa buluu ambapo, ZIPA ilishiriki katika Kongamano la biashara na uwekezaji lililofanyika nchini Mauritius, ilishiriki katika kongamano la nishati, kongamano la mfumo wa chakula Afrika, (AGRF) pamoja na sherehe ya uzinduzi wa mfumo wa usajili miradi (TieW) wa TIC yaliyofanyika Dar es Salaam mwezi wa Septemba. Vile vile, ZIPA ilishiriki katika maonesho ya Swahili International Tourism Expo. Aidha, ZIPA imeendelea kupokea wageni mbali mbali wa wafanyabiashara na wakidiplomasia ambapo ugeni wa balozi wa Tanzania nchini Russia, ugeni wa Balozi wa Tanzania nchini Uingereza, mabalozi wateule wa nchi tofauti pamoja na ujumbe kutoka benki kuu ya Msumbiji.

3) Kushiriki katika ziara za Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Zambia na Norway ambapo pamoja na mambo mengine ya uhusiano fursa za uwekezaji na biashara baina ya Tanzania Zambiana Norway zilijadiliwa;

4) Mamlaka ilishiriki katika kongamano la uwekezaji la Uk - Tanzania Forum lililofanyika nchini Uingereza likiwa ni muendelezo wa makongamano ya UK-Tanzania lenye kuhusisha sekta mbali mbali za mashirikiano ya biashara nafursa za uwekezaji;

5) Mamlaka imefanikiwa kusajili miradi mipya 60 ya uwekezaji ambayo inatarajiwa kutengeneza mtaji wa dola za kimarekani milioni 1,400 na inatarajia kutoa ajira zipatazo 3164;

6) Katika kuendeleza maeneo huru ya Uchumi kwa kuweka miundombinu muhimu ya Barabara Micheweni

Pemba

tayari kampuni ya IRIS inaendelea na ujenzi wa barabarana umekamilika kwa asilimia 100;

7) Mkandarasi ameshamaliza ujenzi wa uzio wa eneo la Micheweni Pemba. Kwa upande wa Eneo la Amaani na Maruhubi mkandarasi ameshaanza kazi za ujenzi wa kituocha maji safi na mitaro ya maji taka.

8) Kukamilisha zoezi la kutambua, kuweka alama pamoja na kuandaa mpango wa matumizi ya Ardhi kwa maeneo ya ardhiza Akiba linaendelea kwa upande wa Unguja na Pemba;

9) Kukamilisha uandaaji wa Sheria na kuanza utayarishaji wa kanuni za Sheria namba 10 ya mwaka 2023 ya Uwekezaji;

10) Kukamilisha utafiti juu ya Mitaji Binafsi ya Wageni (PCF) mzunguko wa 14 ambapo ripoti imeshakamilika na imewailishwa kwenye kamati ya uongozi na tayari imeshapewa ruhusa ya kuisambaza kwa ajili ya matumizi; Aidha, Utafiti huu kwa mzunguko wa 15 umeshaanza kwa kusambaza na kupokea dodoso za taarifa kutoka kwa wawekezaji na hatua inayofuata ni kuchakata taarifa kwa ajili ya kuingiza kwenye mfumo.

11) Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watendaji kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi ambapo wafanyakazi 20 wamepatiwamafunzo ya muda mfupi na wafanyakazi 4 wanaendeleakupatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za shahada na Uzamili kwenye fani mbalimbali ikiwemo Uchumi na Fedha,Ununuzi na Usimamizi wa Rasilimali watu.

## 7.2 PROGRAMU KUU PA0802: UENDESHAJI NA URATIBU WA OFISI KATIKA UCHUMI NA UWEKEZAJI.

75. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kuu kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Bilioni moja, themanini na mbili milioni laki tatu na saba, mia nane na thelathini na nane (TZS.1,082,307,838) mpaka kufikia Machi, 2024 imepatiwa kiasi cha Shilingi Milioni mia saba na sitini na tisa, laki nane na tisini na mbili elfu na themanini na nane (TZS.769,892,088) (matumizi ya kawaida TZS. 303,550,000 na mishahara TZS.466,342,088) sawa na asilimia 71.13 ya utekelezaji program zake ndogo.

### 7.2.1 Programu ndogo SA080201: Utawala na Uendeshaji.

76. **Mheshimiwa Spika;** Programu SA080201 ya Utawala na Uendeshaji ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za uendeshaji na utumishi na kukuza uwezo wa Afisi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Programu ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia Sita na Hamsini na Mbili, Laki Saba na Themanini Elfu, Mia Tatu na Thelathinina Tisa (TZS. 652,780,339) na imeidhinishiwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia Tano na Sitini na Moja, Laki Nne na Arobaini na Moja Elfu, Mia Nne na Sabini na Nane. (TZS. 561,441,478) (matumizi ya kawaida (TZS. 163,050,000) na mishahara (TZS. 398,391,478) ambayo ni sawa na asilimia
86.01 ya makadirio.

77. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2023 – Machi, 2024, Programu ilipanga kusimamia maslahi ya wafanyakazi, kuandaa mpango wa mafunzo ya wafanyakazi ya ndani

na nje, kuimarisha mazingira ya nje na ndani ya afisi na kusimamia ununuzi wa vifaa. Programu hii imetekeleza shughuli zifuatazo: -

1) Imefanya malipo ya umeme, matengenezo ya gari tano, kulipia bima gari tatu na kununua mafuta kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi mbali mbali.

2) Imeratibu na kusimamia maonyesho ya biashara ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyofanyika katika viwanja vya Nyamanzi.

3) Imefanya manunuzi ya vifaa vya ofisi vikiwemo vifaa vya usafi, vifaa vya kuandikia (stationary), samani, AC mbili, mashine ya maji, mifereji, vifaa vya TEHAMA Pamoja na vifaa vya kufanyia matengenezo ya jenereta.

4) Imeratibu kazi ya kuingiza taarifa katika mfumo wa HRMS na kuandaa kuratibu kikao cha Kamati ya Uchumi na kikao cha tano cha zabuni.

5) Imesimamia kuwapatia likizo wafanyakazi sita (6), (Wanaume 2 na Wanawake 4) pamoja na kulipa stahiki zao za posho,

6) Imemlipia mafunzo mfanyakazi mmoja (1) Afisa sheria, Vile vile imewapatia mafunzo wastaafu.

7) Imefanya malipo kwa Mfanyakazi bora, lakini pia imeweza kulipia posho la simu la SNR kwa miezi minne.

8) Imefanya malipo ya posho la bima ya afya kwa wafanyakazi waliopatiwa mafunzo hayo.

9) Imesimamia kuwapatia posho wafanyakazi wa kitengo chausimamizi wa mali kwa ajili ya kuweka barcode.

10) Imelipia posho la ubani kwa wafanyakazi (2) la kufiwa na mzazi.

11) Imelipia Wafanyakazi watano waliaandaa na kukamilishamfumo wa kukusanya taarifa za wafanyakazi kwa mwaka2024/2025 (norminal rol).

12) Imelipia malipo ya saa za ziada (overtime) walinzi 11.

13) Imefanya mafunzo ya Usalama na afya kazini, Kanuni ya Utumishi wa Umma 2014, pamoja na sheria namba 2 ya 2011, Utumishi wa Umma, kwa Wafanyakazi wa ndani.

#### 7.2.2 Programu ndogo SA080201: Uratibu wa Mipango,Sera na Tafiti za Afisi.

**78.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo SA080201: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi kwa kipindi cha Julai, 2023 – Machi, 2024 Programu ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia Mbili na Tisini na Nne, Laki Tatu na Elfu Tisa, Mia Moja na Sabini na Tisa (TZS. 294,309,179) na imeidhinishiwa matumizi ya kiasi cha (TZS. 131,050,610) (matumizi ya kawaida (TZS. 63,100,000 na mishahara (TZS. 67,950,610) sawa na asilimia 44.53.

**79.** **Mheshimiwa Spika,** Programu kwa kipindi cha julai 2023 hadi Machi, 2024 ilipanga kufanya mapitio na uandaaji wa sera, kufanya tafiti, kuratibu utekelezaji wa miradi, ufuatlilaji na tathmini na kuimarisha upatikanaji wa takwimu. Programu hii imetekeleza shughuli zifuatazo: -

1) Imekamilisha uandaaji wa ripoti ya awali (Inception Report) ya utafiti wa mchango wa miradi ya uwekezaji katika kuzalisha ajira kwa Wazanzibari. Utafiti huo utasaidia kutambua hali ya ajira katika miradi ya uwekezaji na kuweka mikakati ya kuimarisha sekta ya uwekezaji Zanzibar.

2) Imeandaa Mpango wa Utekelezaji wa Rasimu ya Sera mpya ya Uwekezaji.

3) Imefanya manunuzi ya vifaa vya kutengenezea mashine ya kutolea fotokopi na manunuzi ya vifaa vya kuandikia (wino wa printa na karatasi).

4) Imefanya kikao cha ushirikiano na Afisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji (SJMT) kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na utaalamu juu ya masuala ya Uwekezaji.

5) Imefanya safari za kikazi Dar es salaam na Dodoma kushiriki katika kikao cha matayarisho na kikao cha maadhimisho yakamati ya miaka 60 ya uhusiano wa kidiplomasia baina yaTanzania na China.

### 7.2.3 Programu ndogo SA080203: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba.

**80. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Afisi Pemba ambayo inahusisha Idara ya Uendeshaji na Utumishi pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Programu ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia Moja na Kumi na Mbili, Laki Nne na Themanini (TZS. 112,480,000) hadi

kufikia mwezi Machi, 2024, Programu imeingiziwa Shilingi Milioni Sabini na Saba na Laki Nne (TZS. 77,400,000) sawa na asilimia 57.24 ya makadirio.

81. **Mheshimiwa Spika,** Programu kwa kipindi cha Julai, 2023 – Machi, 2024 ilipanga kurusha hewani vipindi na kufanya makongamano, kutayarisha dhana za miradi ya PPP Pamoja na kutoa taaluma kwa taasisi, kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na miongozo, itatoa mafunzo, ununuzi wa vifaa na kuandaa taarifa za utekelezaji. Programu hii imetekeleza yafuatayo: -

1) Imefanya manunuzi ya mafuta, chakula na vinywaji, vifaa vya kuandikia, vifaa vya usafi na kulipia gharama za umeme, maji na huduma ya mtandao na huduma ya usafi. Pia, imelipia gharama za safari kwa maafisa waliokwenda Unguja kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kazi za Afisi na kuwajengea uwezo watendaji wawili (2) wanawake katika kada ya uandishi wa habari. Vile vile imelipia fedha za ubani kwa mfanyakazi mmoja (1) mwanaume aliefiliwa na babayake mzazi na posho la likzo kwa mfanyakazi mmoja.

2) Imeandaa na kurushwa hewani vipindi vitano (5), kupitia Televisheni na Redio; Makala mbili (2) na Stori 7 zimeandaliwa. Aidha, inaendelea kukamilisha Jarida la “Uwekezaji Pemba” ambalo litaeleza kazi na mafanikio yaProgramu ya Uchumi na Uwekezaji.

3) Imefanya makongamano manne (4) kwa Vijana wa vyuo vya amali Daya Mtambwe, Vitongoji na Chuo cha elimu Mbadala Wingwi Micheweni na Jumuia za vijana kuhusu Sekta ya Uchumi na Uwekezaji katika

kutengeneza fursa

za ajira kwa Vijana. Jumla ya washiriki 281 (Wanawake 145 na Wanaume 136) walihudhuria. Kupitia makongamano hayo, vijana walijifunza na kuzitambua fursa mbalimbali zinazopatikana katika Sekta ya Uchumi na Uwekezaji zikiwemo ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja. Aidha, makongamano hayo yalitumika kubadilisha fikra za vijana za kutegemea kazi kutoka Serikalini pekee na kuwahamasisha kutumia fursa zilizopo kujiajiri.

4) Imefanya ufuatiliaji kwa lengo la kuboresha utendaji wa shughuli za Afisi. Pia, ilitayarisha ripoti za ufuatiliaji na tathmini ambazo zinaonesha mafanikio, changamoto na mapendekezo. Ufuatiliaji huo ulifanyika katika miradi ya Hoteli, Maeneo huru ya Uwekezaji Micheweni, Viwanda vya maji Maeneo ya Visiwa vilivyopata Wawekezaji ikiwemo Kisiwa cha Kuji na Matumbini kuona hatua mbali mbali zinazofanywa na Wawekezaji sambamba na kufuatilia utekelezaji wa miongozo inayotolewa. Kwa upande wa Hoteli zilizofuatiliwa ambazo zinatoa huduma, matokeo yanaonyesha kuwa zinaendelea na huduma vizuri na wanafuata masharti na utaratibu wa kisheria katika uendeshaji wa shughuli zao. Kwa upande wa maeneo huru ujenzi wa barabara za ndani umekamilika. Aidha, ufuatiliaji umebaini uharibifu wa barabara unaofanywa na wananchi kwa kungoa baadhi ya alama za barabarani. Baada ya ufuatiliaji huu Afisi imechukua hatua ya kuzungumza na wananchi sambamba na kurusha kipindi maalum na kutoa matangazo kupitia redio jamii Micheweni kuhamasisha wananchi kulitumia Eneo vizuri kwa maslahi ya jamii naTaifa kwa jumla.

5) Imeratibu ziara maalum ya Dar es Salaam kwa lengo la kufanya uenezi juu ya fursa na vivutio maalum vya uwekezaji katika kisiwa cha Pemba, kujifunza shughuli mbalimbali za wawekezaji,kufanya ulinganisho wa Uwekezaji wa Zanzibar na Tanzania Bara, Kusikiliza changamoto mbalimbali za wawekezaji kwa lengo kuweka mazingira rafiki ya kuondoa changamoto hizo kabla ya kuekeza Zanzibar.Maeneo yaliyofikiwa ni Kinglion Misugusugu –Kibaha, GF Trucks TAMCO, East Africa Commercial and Logistic Center – Ubungo,Kampuni ya ALAF (Safal Group) - Nyerere Road naKiwanda cha Maisha Bottlers.

6) Imewajengea uwezo watendaji kwa kuwapatia mafunzo ya juu ya dhana ya miradi ya PPP na maswala ya Usalama na Afya Kazini ambapo jumla ya watendaji 38 (Wanawake 19 na Wanaume 19) walishiriki. Elimu hiyo itawasaidia kutatua changamoto mbali mbali za kiafya na kiusalama katika maeneo yao ya kazi, aidha watakuwa ni mabalozi wazuri katika kuwasaidia wafanyakazi wengine kuwapatia taaluma hio. Vile vile, imetoa mafunzo ya uandaaji wa ripoti mbali mbali kwa watendaji 30 (Wanawake 13 na Wanaume 17) wa Afisi ili kuwasaidia watendaji kuwa na mfumo unaofanana katika uandishi wao wa ripoti kulingana na ainaya ripoti inayohitajika. Aidha, imetoa mafunzo ya E- Office kwa wafanyakazi 26 (Wanawake 14 na Wanaume 12)

7) Imeshiriki maonyesho ya chakula duniani yaliyofanyika Chamanangwe Pemba kwa lengo la kutangaza shughuli zaAfisi kwa wananchi kupitia maonesho hayo.

8) Imeratibu utayarishaji wa ripoti mbali mbali ikiwemo ripoti za utekelezaji kwa vipindi tofauti, utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 - 2025 na utekelezaji wa maagizo ya viongozi.

## 8.0 MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.

## 8.1 VIPAUMBELE VYA AFISI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

82. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji imepanga kutekelezavipaumbele vifuatavyo: -

1) Kuratibu upatikanaji wa ajira za staha 3500 nje ya nchi na ajira rasmi 15,000 za ndani pamoja na kukuza ujuzi kwa Vijana 110 kuweza kujiajiri na kuajirika; Kuimarisha Usalama na Afya kazini kwa ununuzi wa vifaa vya uchunguzi; kufanya ukaguzi kazi katika maeneo ya kazi 600 (Unguja 500 na Pemba 100) na kuimarisha majadiliano na kutatua migogoro ya kazi 162.

2) Kuimarisha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kufanya mageuzi ya vyama vya ushirika; kutoa mikopo nafuu kwa wajasiriamali 26,000 kwa kuongeza program za uwezeshaji; kulea na kukuza wajasiriamali kwa kujenga kituo kimoja, kutoa mafunzo kwa wajasiriamali 8,612 na kuwaunganisha na masoko wajasiriamali 450 na kuimarisha viwanda vidogovidogo na vya kati.

3) Kukuza na kuimarisha Uwekezaji kwa kuweka mikakati ya kutangaza fursa na kusajili miradi ya Uwekezaji 110; miradi ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), kuimarisha miundombinu ya ujenzi wa Barabara za ndani katika zoni B Eneo la Micheweni na kuanza na ujenzi wa Ofisi eneo la Mazizini.

4) Kufanya mageuzi ya ARKUU kwa kuimarisha mazingira ya kazi (nyenzo, kukuza ujuzi wa wafanyakazi na kuweka

mazingira wezeshi ya kazi), kukuza maslahi ya wafanyakazi pamoja na kutumia mifumo ya kidijitali.

5) Kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, kufanya mapitio ya Sera na Sheria ya PPP, kuandaa Sera ya Local Content, Sheria ya Ajira, Kukamilisha Kanuni zinazotokana na Sheria ya Uwekezaji, kuimarisha Ufuatiliaji na kufanya Tafiti pamoja na kukuza uwelewa kwa jamii juu ya utekelezaji wa majukumu ya ARKUU.

## 9.0 MUELEKEO WA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.

### 9.1 MAPATO.

**83.** **Mheshimiwa Spika**, Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 imepangiwa kukusanya jumla ya (TZS 6,695,420,000) kutoka fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) kupitia vianzio vyake vinne (4) vikiwemo Ada za Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi, Ada ya Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi. **(Kiambatanisho nambari 6 kinahusika).**

### 9.2 MATUMIZI

**84.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji ili iweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kupitia Fungu A07, A08 na A11; inaombewa kutumia jumla ya TZS. 75,206,100,000 Kati ya fedha hizo Shilingi (TZS. 4,971,500,000) ni Mishahara; (TZS. 5,810,800,000) ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida; (Tsh. 848,800,000) kwa ajili ya matumizi ya ruzuku; (TZS.

4,975,000,000) ni ruzuku ya Mishahara. Pia, Afisi inaliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya shilingi bilioni hamsini na moja, milioni mia tano (TZS. 51,500,000,000) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kutoka Fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na TZS 7,100,000,000 kutoka kwa Washirikawa Maendeleo. **(Viambatanisho nambari 7 a na b vinahusika).**

85. **Mheshimiwa Spika,** Afisi kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) ili iweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisikwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Saba Milioni Mia mbili Sabini na tatu, na laki tatu (TZS 7,273,300,000). Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni mbili, milioni mia moja na tisini na tatu (Tsh.2,193,000,000) ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida; Shilingi milioni mia nane arobaini na nane na laki nane (Tsh.848,800,000) ni ruzuku ya matumizi ya kawaida; na Shilingi bilioni mbili, milioni mia tisa na mbili na laki tatu (TZS 2,902,300,000) kwa Mishahara na Shilingi Bilioni Moja, Milioni mia mbili na thelathini na tisa na laki mbili (Tsh.1,239,200,000) ni ruzuku ya Mishahara.

86. **Mheshimiwa Spika,** Mgawanyo wa matumizi ya fedha hizo kwa Programu za fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) ni kama ifuatavyo: -

    1) Programu Kuu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote, (ina Programu Ndogo tatu zikiwemo Programu Ndogo ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Afya na Usalama Kazini, na Programu Ndogo ya Usimamizi wa

Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja) Ili Programu itekeleze majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya ruzuku ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja na Sabini na nane Elfu (TZS.2,178,000,000) kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara. kati ya hizo Shilingi milioni mia nane na arobaini na nane na laki nane (TZS 848,800,000) ya kazi za kawaida na Shilingi Bilioni Moja, Mia tatu ishirini na tisa na Laki mbili (TZS1,329,200,000) ikiwa ni ya Mishahara.

2) Programu Kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ina Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa vyama vya Ushirika). Ili Programu itekeleze majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni moja milioni themanini laki saba ishirini na tano elfu (TZS.1,080,725,000) kati ya hizo Shilingi Milioni Mia sita kumi na tano na laki mbili (TZS 615,200,000) kwa Matumizi ya kawaida, Shilingi Milioni mia nne sitini na tano, laki tano na ishirini na tano elfu (TZS. 465,525,000) za Mishahara.

   i. Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji (ina Programu Ndogo tatu zikiwemo Program Ndogo ya Uratibu wa Sera, Mipango na Tafiti, Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji na Program Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba). Ili Programu itekeleze majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni tatu, Milioni Mia tano sitini na tano, Laki saba na arobaini na

sita Elfu (TZS.3,565,746,000) kati ya hizo ni Bilioni moja milioni mia tano sabini na saba na laki nane (TZS 1,577,800,000) kwa ajili Matumizi ya kawaida na Shilingi Bilioni moja milioni mia nane arobaini na mbili, laki nne sabini na tano elfu (1,842,475,000) kwa ajili ya Mishahara (**Kiambatanisho nambari8 a kinahusika**).

87. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imehamishiwa fungu A11. Ili Programu itekeleze majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe Shilingi Bilioniarobaini na Sita, milioni mia nane sabini na tisa na Laki saba (TZS. 46,879,700,000) ambapo shilingi Bilioni mbili, milioni ishirini na mbili TZS. 2,022,000,000 ni kwa Matumizi ya kawaida, shilingi Bilioni moja, milioni mia mbili Hamsinina Saba na laki saba (TZS. 1,257,700,000) kwa ajili ya mishahara na shilingi Bilioni Arobaini na tatu na Milionimia sita (TZS. 43,600,000,000) kwa kazi za maendeleo. (**Kiambatanisho nambari 8 b kinahusika)**.

88. **Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya kuwawezesha wananchi kuchumi ina Programu Ndogo moja ya Kuwawezesha Wananchi. Ili Programu itekeleze majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya ruzuku ya Shilingi Bilioni arobaini nan ne, milioni mia moja sitini na saba, laki moja na ishirini na tano elfu (TZS. 44,167,125,000 ambapo TZS. 567,125,000 matumizi ya kawaida na TZS. 43,600,000,000 kwa ajili ya miradi ya Maendeleo)

89. **Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya Utumishi na Uendeshaji wa Taasisi ya ZEEA ina Programu Ndogo mbili, Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji na Programu ya Afisi Kuu Pemba. Ili Programu itekeleze majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Barazalako liidhinishe jumla ya ruzuku ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Saba kumi na mbili Laki tano sabini na tano elfu (TZS. 2,712,575,000 ambapo TZS. 1,454,875,000 matumizi ya kawaida na TZS. 1,257,700,000 kwa ajili ya mishahara)

## 10.0 MUELEKEO WA MATUMIZI KWA KILA PROGRAMU

## 10.1 FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)

90. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha kwa mwaka wa fedha 2024/2025, imepanga kutekeleza yafuatayo: -

1) Kuendeleza programu maalum ya kukuza ujuzi kwa vijana Wasio na Ajira, Elimu na Hawapo katika Mafunzo yoyote (NEET Program) iliokuwa ikitekelezwa kwa mashirikiano naShirika la Kazi Duniani ILO;

2) Kusimamia uandaaji wa Mfumo wa Taarifa za Soko la Ajira utakaotoa matokeo muhimu ya viashiria vya Soko la Ajira;

3) Kuendelea na Kuimarisha mashirikiano na wadau Pamoja na kuratibu upatikanaji wa fursa za Ajira za ndani na nje ya Nchikwa kushirikiana na Taasisi za Uwakala Binafsi wa Ajira;

4) Kuendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya ajira kupitia majukwaa tofauti ikiwemo makongamano, vipindi vya redio

nk.;

5) Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Utekelezaji wa Ajira kwa Vijana (Zanzibar Youth Employment Action Plan) unaolenga kuzalisha fursa za ajira kwa wingi katika sekta tofauti na

6) Kufanya mapitio ya Kanuni za Wakala Binafsi wa Ajira ya mwaka 2012 ili kuleta ufanisi wa shughuli zao pamoja na kuandaa kanuni ya kusimamia Mfumo wa Taarifa za Ajirakwa watafuta kazi (Jobseeker Portal).

91. **Mheshimiwa Spika,** Ili Programu ya Ndogo ya Uratibu na Upatikanaji wa Ajira za Staha iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe ruzuku ya jumla ya Shilingi Milioni Mia Mbili na Sitini (TZS. 260,000,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

92. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kaziniimepanga kutekeleza yafuatayo: -

1) Kuzifanyia ukaguzi sehemu 240 za kazi ili kuhakisha kuwa taratibu za kisheria kuhusia na masuala ya usalama na afyakatika sehemu za kazi zinafuatwa.

2) Kutoa maelekezo na Mafunzo kwa Taasisi za Umma 35 na binafsi 45 kuhusu masuala ya Usalama na Afya katikasehemu za kazi.

3) Kuzitambua, kuzisajili sehemu 160 za kazi na kuweka kumbukumbu za Usalama na Afya kazini kwa mujibu wa Sheria ya Usalama na Afya namba 8 Ya 2005

4) Kuimarisha maslahi ya watendaji wa Idara kwa ujumla

5) Kuandaa miongozo ya (kanuni 3 za Usalama na afya kazini) utekelezaji wa masuala ya usalama na afya kazini.

93. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Naliomba Baraza lako liidhinishe ruzuku ya Shilingi Milioni Mia Mbili Arobaini na Saba na Ishirini Elfu (TZS. 247,020,000/-) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na mishahara.

94. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja, mbali na majukumu mengine itatekeleza yafuatayo: -

1) Kuendelea kufanya ukaguzi wa maeneo ya kazi Unguja na Pemba kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa sheria zakazi;

2) Kuanzishwa kwa mfumo wa kuhifadhi na kusambaza taarifaza shughuli zote za kazi (labour case management system) kwa lengo la kuwepo kwa uhifadhi na upatikanaji kwa urahisi wa taarifa husika;

3) Kutoa elimu kwa Waajiri na wafanyakazi juu ya haki, sheria za kazi na wajibu wanapokuwa katika sehemu zao za kazi;

4) Kwa kushirikiana na Vyuo vya Elimu ya Juu (Higher Learning Institutions) kuanzisha programu maalum za masuala ya kazi/mahusiano kazini (Labour Relations Training Programs);

5) Kuimarisha huduma za Utoaji wa vibali kwa wafanyakazi wa kigeni wanaokuja kufanya kazi Nchini;

6) Kuimarisha Kamisheni ya Kazi kwa Kuwajengea uwezo wa taaluma ya ukaguzi wa maeneo ya kazi, utatuzi wa malalamiko na migogoro ya kazi na upatikanaji wa nyenzo za ufanyaji kazi pamoja na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika kada mbalimbali.

7) Kuandaa vikao vya kuimarisha ushirikiano na Jumuiya za Wafanyakazi na Waajiri na Kuendelea kukagua vyama vyaWafanyakazi na Waajiri.

95. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Naliomba Baraza lako liidhinishe ruzuku ya Shilingi Bilioni Moja Milioni Mia Sita Sabini na laki tisa na themanini Elfu (TZS. 1,670,980,000/-) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na mishahara.

96. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu ya Usimamizi na Uimarishaji wa vyama vya Ushirika imepanga kutekeleza yafuatayo: -

1) Kusajili Vyama Vya Ushirika 1,800 (Unguja 1,200 na Pemba 600);

2) Kukagua hesabu za Vyama vya Ushirika 500 Unguja (300) na Pemba (200);

3) Kufuatilia na kufanya uchunguzi kwa vyama vya ushirika 1000 Unguja (600) na Pemba (400);

4) Kutoa mafunzo kwa wanachama na 16,000 kutoka kwenye Vyama 2,300 vya Ushirika;

5) Kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa usajili na Usimamiziwa vyama vya Ushirika na

6) Kufanya utafiti mdogo juu ya mageuzi ya sekta ya Ushirika Zanzibar.

97. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Themanini, Laki Saba na Ishirini na Tano Elfu (TZS.1,080,725,000) kati ya hizo Shilingi Milioni Mia Sita na Kumi na Tano Laki Mbili (TZS 615,200,000) kwa Matumizi ya kawaida na Shilingi Milioni Mia Nne Sitini na Tano, Laki Tano Ishirini na Tano Elfu (TZS. 465,525,000) kwa mishahara.

98. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu Program Ndogo ya Uratibu wa Sera, Mipango na Tafiti Program Ndogo ya Uratibu wa Sera, Mipango na Tafiti imepanga kutekeleza yafuatayo:-

1) Kufanya tafiti za Afisi kwa mujibu kwa ajenda ya Utafiti;

2) Kuratibu utekelezaji wa mipango, programu na miradi ya Afisi;

3) Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Afisi;

4) Kuandaa na kufanya mapitio ya sera zinazohusiana na Afisi;

5) Kuimarisha upatikanaji wa takwimu za shughuli mbali mbali za Afisi na

6) Kuimarisha mashirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

**99. Mheshimiwa Spika,** Ili Program Ndogo ya Uratibu wa Sera, Mipango na Tafiti za Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako kupitisha jumla ya Shilingi Milioni Mia Sita na Tatu, Laki Nane na Themanini na Saba Elfu (TZS. 603,887,000) Matumizi ya kawaida ni Shilingi Milioni Mia Tatu na Sabini na Laki Moja (TZS. 370,100,000) na mishahara ni Shilingi Milioni Mia Mbili na Thelathini na Tatu, Laki Saba na Themanini na Saba Elfu (TZS. 233,787,000) kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mishahara.

**100. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji imepanga kutekeleza yafuatayo: -

1) Kuimarisha maslahi ya wafanyakazi kwa kuwapatia stahikina maposho.

1) Kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kiutendaji pamoja nakuwapatia nyenzo za kufanyia kazi.

2) Kuwezesha safari za kikazi nje na ndani ya nchi.

3) Kuimarisha huduma za uendeshaji na utawala.

101. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja na Ishirini na Tatu na Elfu Kumi na Nne (TZS.2,123,014,000)(Matumizi ya kawaida Shilingi Milioni Mia Sita na Hamsini na Saba (TZS. 657,000,000) na mishahara Bilioni Moja, Milioni Mia Nne na Sitini na Sita na Elfu Kumi na Nne (TZS. 1,466,014,000.) kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mishahara.

102. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba imepanga kutekeleza yafuatayo: -

2) Itasimamia na kuimarisha Maslahi ya Wafanyakazi kwakuwapatia stahiki na maposho.

3) Itajenga na Kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kiutendaji pamoja na kuwapatia nyenzo za kufanyia kazi.

4) Itaandaa Mpango wa Mafunzo na Mpango wa Rasilimaliwatu;

5) Itasimamia na Kuimarisha huduma za uendeshaji na utawala.

6) Itafanya ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli za Afisi Pemba na itaimarisha upatikanaji wa takwimu.

7) Itafanya tathmini ya vyama vya SACCOS na kuandaa maandiko ya miradi:

8) Itaratibu uandaaji wa ripoti za utekelezaji (Ilani, PDB, Hotuba, PBB, MTEF) mbali mbali kwa mujibu wa maagizo:

9) Kuimarisha Mashirikiano ya Kitaifa pamoja na kutoa elimukupitia vyombo vya habari kuhusiana na shughuli mbalimbali zin azotekelezwa na Afisi.

**103. Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Uratibu na Utekelezajiwa Shughuli za Afisi Pemba iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili na Themanini na Saba, Laki Sita na Sabini na Nne Elfu (TZS. 1,287,674,000) matumizi ya kawaida ni Shilingi Milioni Mia tano na hamsini, Laki Saba (TZS 550,700,000 na mishahara ni Shilingi Milioni Mia saba Thelathini na sita, Laki tisa na sabini na nne elfu (TZS 736,974,000).

## 10.2 FUNGU A11 WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

**104. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imepanga kutekeleza yafuatayo: -

1) Kutoa taaluma kwa Mamlaka 7 za Serikali za Mitaa kuhusiananana taratibu za mikopo.

2) Kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wananchi 18,000.

3) Kufanya ushajihishaji wa matumizi ya fedha kimtandao kwa Wajasiriamali, Wazalishaji na Wafanyabiashara 200.

4) Kutoa Mafunzo kwa Wajasiriamali, wazalishaji na wafanyabiashara 2,600 kuhusiana na fani mbali mbali zikiwemo usarifu wa mazao, ufugaji wa nyuki wa asali, masoko, na usimamizi wa fedha.

5) Kuwaunganisha Wajasiriamali, Wazalishaji na Wafanyabiashara 210 na fursa za masoko kupitia makongamano na wamiliki wa mahoteli na kuwasaidia kushiriki maonesho.

6) Kuwaunganisha Wajasiriamali na wazalishaji 60 na Taasisiza ubora na Viwango.

7) Kusaidia ukuaji wa viwanda 120 kutoka hatua ya viwanda vidogo vidogo kuwa vidogo, vidogo kuwa vya kati.

8) Kutoa huduma za kiufundi na ushauri wa kitaalamu kwa viwanda 50 vidogo vidogo, vidogo na vya kati.

105. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe Shilingi Bilioni Arobaini na Nne, Milioni MiaMoja na Sitini na Saba, Laki Moja na Ishirini na Tano Elfu (TZS. 44,167,125,000) ambapo Shilingi Milioni mia tano sitini na Saba, laki Tisa na Thelathini Elfu (TZS. 567,125,000) ni kwa Matumizi ya kawaida, na Shilingi Bilioni Thelathini na sita na Milioni Mia tano (TZS. 36,500,000,000) za kazi za maendeleo (TZS. 30,000,000,000 za Programu ya INUKA,TZS 4,500,000,000 za mfuko wa Khalifa kutoka SMZ na TZS. 2,000,000,000 za Mifumo ya Ofisi na 7,100,000,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya mradi wa

Mfuko wa Khalifa na mradi wa Pamoja wa Benki ya Dunia **(Kiambatanisho nambari 8 b kinahusika).**

106. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu ndogo ya utumishi na uendeshaji imepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo: -

1) Kuimarisha maslahi ya wafanyakazi kwa kuwapatia stahikina maposho.

2) Kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kiutendaji pamoja nakuwapatia nyenzo za kufanyia kazi.

3) Kuwezesha safari za kikazi ndani ya nchi (Pemba na TanzaniaBara).

4) Kuimarisha huduma za uendeshaji na utawala.

5) Kuratibu masuala ya uwezeshaji nchini kupitia Wizara zote na Taasisi binafsi.

6) Kufanya tafiti moja (1) katika maeneo ya uwezeshaji.

7) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa wanufaika 400 wa huduma za uwezeshaji.

8) Kuelimisha jamii kuhusiana na masuala ya uwezeshaji kupitia vipindi 10 vya TV na 10 vya Redio, aidha kupitia mitandao ya kijamii na majarida.

9) Kutayarisha mifumo mitatu (3) muhimu ya kielektroniki itakayosaidia kurahisisha utendaji wa kazi.

107. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi iuchumi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tisa na Themanini na Tano, Laki Mbili na Kumi na Saba Elfu (TZS. 1,985,217,000) ambapo Shilingi Milioni Mia Tisa na Hamsini na Tano, Laki Mbili na Sabini na Tano Elfu (TZS. 955,275,000) kwa matumizi ya kawaida na Shilingi Bilioni Moja, Milioni Ishirini na Tisa, Laki Tisa na Arobaini na Mbili Elfu (TZS. 1,029,942,000) kwa ajili ya mishahara. **(Rejea Kiambatatanisho nambari 8b)**

### 10.2.1 Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wakala Pemba

108. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wakala Pemba imepanga kutekeleza malengomakuu yafuatayo:

1) Kutoa taaluma kwa Mamlaka 4 za Serikali za Mitaa kuhusiana na taratibu za mikopo.

2) Kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wananchi 8,000.

3) Kutoa Mafunzo kwa Wajasiriamali, wazalishaji na wafanyabiashara 2,150 kuhusiana na fani mbali mbali zikiwemo usarifu wa mazao, ufugaji wa nyuki wa asali, masoko, na usimamizi wa fedha.

4) Kuwaunganisha Wajasiriamali, Wazalishaji na Wafanyabiasha 240 na fursa za masoko kupitia

makongamano na wamiliki wa mahoteli na kuwasaidia kushiriki maonesho.

5) Kuwaunganisha Wajasiriamali na wazalishaji 60 na Taasisi za ubora na Viwango.

6) Kusaidia ukuaji wa viwanda 80 kutoka hatua ya viwanda vidogo vidogo kuwa vidogo, vidogo kuwa vya kati.

7) Kutoa huduma za kiufundi na ushauri wa kitaalamu kwa viwanda 50 vidogo vidogo, vidogo na vya kati.

8) Kuimarisha maslahi ya wafanyakazi kwa kuwapatia stahiki na maposho.

9) Kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kiutendaji pamoja na kuwapatia nyenzo za kufanyia kazi.

10) Kuwezesha safari za kikazi ndani ya nchi (Unguja na Tanzania Bara).

11) Kuimarisha huduma za uendeshaji na utawala.

12) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli za Afisi Pemba na kuimarisha upatikanaji wa takwimu.

13) Kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa pamoja na kutoa elimu kupitia vyombo vya habari kuhusiana na shughuli mbali mbali zinazotekelezwa na Afisi.

109. **Mheshimiwa Spika ,** Programu ndogo ya Uratibu wa Afisi ya Wakala Pemba ili iweze kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi

Milioni Mia Saba Ishirini na Saba, Laki Tatu na Hamsini na Nane Elfu (TZS. 727,358,000) ambapo Shilingi Milioni Mia Nne Tisini na Tisa na Laki Sita (TZS. 499,600,000) kwa matumizi ya kawaida na Shilingi Milioni Mia Mbili Ishirini na Saba, Mia Saba na Hamsini na Nane Elfu (TZS. 227,758,000) kwa ajili ya mishahara.

## 10.3 FUNGU A08 UCHUMI NA UWEKEZAJI

**110. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) ili iweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Ishirini na Moja, Milioni Hamsini na Tatu na laki moja (TZS.21,053,100,000) Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Moja miilioni mia tano na tisini na tano elfu na laki nane (TZS. 1,595,800,000) ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za Kawaida; Shilingi Milioni nane kumi na moja elfu na laki tano (TZS. 811,500,000) ni kwa ajili ya Mishahara; Shilingi Bilioni tatu, Milioni Mia sita arubainina tano na laki nane (TZS.3,645,800,000) ni kwa ajiliya Ruzuku ya Mishahara na Shilingi Bilioni kumi na tano (TZS.15,000,000,000) kutoka SMZ kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. **(Kiambatanisho Nambari 8 ckinahusika)**

**111. Mheshimiwa Spika,** Mgawanyo wa fedha hizo kwa Programu za Fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) ni kama ufuatao: -

### 10.3.1 MUELEKEO WA MATUMIZI KWA KILA PROGRAMU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI).

112. **MheshimiwaSpika;** Program Ndogo ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Kwa mwaka wa fedha 2024/25 itatekeleza yafuatayo; -

1) Itaratibu miradi ya PPP (Kupitia maandiko ya awali, upembuzi yakinifu awali na kamilifu na vikao vya wadau).

2) Itashiriki mikutano inayohusu mambo ya PPP Tanzania Bara na nje ya nchi.

3) Itazitembelea Mamlaka za utekelezaji pamoja na maeneo yaliyotengwa au kuibuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya PPP ili kutambua hatua iliyofikiwa na changamoto na kuandaa mpango wa kutatua changamoto hizo.

4) Itajenga uwezo kwa wafanyakazi wa PPP na mamlaka za utekelezaji kuhusu mambo ya PPP (model za kifedha, uchambuzi wa mazingira, ufuatiliaji na tathmini na manunuzi) pamoja na ununuzi wa vifaa/nyenzo.

5) Itarekebisha Sheria na kanuni ya PPP na itaandaa muongozo wa PPP unaowashirikisha wananchi.

6) Itafuatilia na kufanya tathmini ya miradi ya PPP.

7) Itatayarisha models documents and PPP tools.

8) Itafanya na kuhudhuria Mijadala Baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi.

113. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Ndogo ya Mashirikiano Baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Saba na Sitini na Mbili, Elfu Sitini na Nane na Mia Nne (TZS. 762,068,400) ni matumizi ya kawaida ya Shilingi Milioni mia sita na thelathini na nne, laki nane na thelathini elfu (TZS. 634,830,000) Na mishahara ni Shilingi Milioni Mia moja na ishirini na saba, laki mbili, thelathini na nane elfu na mia nne (TZS. 127,238,400).

114. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 Programu Ndogo ya Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji itatekeleza yafuatayo: -

1) Kuendelea na shughuli za uenezi ambazo zinahusisha mikutano, makongamano, maonesho na ziara mbalimbali za kimataifa na kitaifa (Promotion) zinazoendana na vipaumbele vya sera ya Uchumi wa buluu;

2) Kuendelea na awamu ya pili ya uendelezaji wa mfumo wa kieletronikali kuwahudumia Wawekezaji;

3) Kusajili miradi ya uwekezaji 110 ambayo inatarajiwa kuingiza mtaji wa dola za kimarekani milioni 2,000 na makisio ya ajira 3,250;

4) Kuanza Ujenzi wa barabara za ndani katika Zoni B eneo la Micheweni Pemba;

5) Kuendela kufanya utafiti juu ya mitaji binafsi (PCF) mzunguko wa 16;

6) Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi yanayoendana na majukumu wafanyakazi wa Mamlaka;

7) Kuandaa mkakati wa uenezi na wa mawasiliano waMamlaka ya Kukuza Uwekezaji.

115. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2024/2025 inatarajia kukusanya jumla ya TZS 4,421,737,313.34. Na kwa upande wa matumizi Mamlaka imepanga kutumia jumla TZS 3,710,355,038 kwa matumizi ya kawaida.

116. **Mheshimiwa Spika,** Ili Programu Ndogo ya Maendeleoya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe Shilingi Bilioni Kumi na Nane, Milioni Mia Sita na Arobaini na Tano, na Laki Nane (TZS. 18,645,800,000) Ruzuku ya mishahara ni Shilingi Bilioni Tatu, Milioni mia sita na arubaini na tano na laki nane (TZS. 3,645,800,000) na Fedha za maendeleo kutoka SMZ ni Shilingi Bilioni Kumi na tano (TZS. 15,000,000,000).

117. **Mheshimiwa Spika,** Programu Programu Ndogo ya ya Utawala na Uendeshaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu itatekeleza yafuatayo: -

1) Kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kwa kuwapatia stahiki na maposho.

2) Kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kiutendaji.

3) Kuwezesha safari za kikazi nje na ndani ya nchi.

4) Kuimarisha huduma za uendeshaji na utawala.

118. **Mheshimiwa Spika,** Ili Programu Ndogo ya ya Utawalana Uendeshaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Ishirini na Tatu, Laki Nne na Elfu Mbili (TZS. 1,023,402,000) Matumizi ya kawaida ni shilingi Milioni mia nne, sitini na tano na laki tano tisini elfu (TZS. 465,590,000) na mishahara ni Shilingi Milioni Mia tano Hamsini na saba, laki nane na kumi na mbili elfu (TZS. 557,812,000) kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mishahara.

119. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu Ndogo ya Uratibu wa Sera, Mipango na Utafiti itatekeleza yafuatayo:

1) Kufanya mafunzo ya Utafiti kwa watendaji wa Afisi;

2) Kuwajengea uwezo watendaji wa Idara kwenye maeneo yao ya kazi;

3) Kuratibu utekelezaji wa mipango, programu na miradi ya Afisi;

4) Kuandaa na kufanya mapitio ya sera zinazohusiana na Afisi na

5) Kuimarisha upatikanaji wa takwimu za shughuli mbali mbali za Afisi na kuimarisha mashirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

120. **Mheshimiwa Spika,** Ili Programu Ndogo ya Uratibu wa Sera, Mipango na Tafiti za Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi (TZS. 435,850,600). (Matumizi ya kawaida 342,380,000 Na mishahara 93,470,600.) kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mishahara.

121. **Mheshimiwa Spika,** Program kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 itatekeleza yafuatayo:

1) Kuratibu utekelezaji wa Programu na Miradi ya Afisi.

2) Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Afisi.

3) Kuendelea kufanya Uenezi wa Uwekezaji (Uwekezaji binafsi na Wa mashirikiano PPP).

4) Kuimarisha upatikanaji wa takwimu za shughuli mbali mbali za Afisi na Kuimarisha Mashirikiano ya Kitaifa.

5) Kuendelea kusimamia utekelezaji bora wa sera, sheria na miongozo mbalimbali kwa kusimamia maslahi ya wafanya kazi kwa kulipa posho ya safari, malipo ya masaa ya ziada, likizo wafanyakazi, huduma ya mazishiwafanyakazi na matibabu wafanyakazi.

6) Kuwajengea uwezo wafanyakazi katika mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

7) Kulipia gharama za maji, umeme na huduma ya usafi na itafanya manunuzi ya mafuta, vifaa vya kuandikia, vifaa vya usafi na kumpyuta.

8) Itaandaa Mpango wa Mafunzo na Mpango wa Rasilimali watu, zoezi la Upimaji Utendaji kazi kwa Wafanyakazi kwa kila mwaka na kusimamia suala la uajiri wa Wafanyakazi.

122. **Mheshimiwa Spika,** Ili Programu ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 Naliomba Baraza lako liidhinishe Shilingi Milioni Mia Moja na Themanini na Tano, Laki Tisa na Sabini na Tisa Elfu na Tisini na Nne (TZS. 185,979,094) (Matumizi ya kawaida (TZS. 153,000,000) na mishahara 32,979,094)kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

## 11.0 SHUKURANI.

123. **Mheshimiwa Spika;** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji inatanguliza shukurani zake za dhati kwa mashirikiano mazuri kupitia taasisi mbali mbali zinazofanya kazi pamoja zikiwemo Taasisi za Serikali, Taasisi Binafsi, Washirika wa Maendeleo, Mabenki, Asasi za Kiraia, Wakuu wa Mikoa, Wakuu Wa Wilaya na Jamii kwa ujumla. Afisi inaanza kwa kuwashukuru Washirika wa Maendeleo tunaofanya kazi nao ambao ni ILO, UNDP, FAO, Benki yaDunia (World Bank), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, inazishukuru taasisi za kiraia ikiwemo ZATUC, ZANEMA COSTECH, Chuo cha Ushirika Moshi, Milele Foundation na Taasisi zote zinazoshirikiana nasi kwani si rahisi kuzitaja moja moja. Pia, Afisi inazishukuru Taaasisi zote za kifedha ikiwemo Benki ya PBZ, Equity Benki, AMANA Benki, ADB, TABD,

DTB, BOA, CRDB Benki na Taasisi zote za Fedha zikiwemo SACCOS kwa mashirikiano yao mazuri na Afisi yetu. Vile vile tunawaomba Washirika wa Maendeleo wengine kujitokeza kusaidia juhudi za Serikali kwenye Sekta hizi muhimu za Kazi na Ajira, Uwezeshaji na Uwekezaji.

124. **Mheshimiwa Spika;** Aidha, Napenda kuvishukuruvyombo vyote vya habari vinavyoshirikiana nasi katika kuelimisha jamii juu ya shughuli zinazozifanywa na Afisi. Vyombo hivyo vimechangia kwa kiasi kikubwa shughuli za Afisi yetu kujulikana na jamii. Sitaweza kuvitaja kimoja kimoja lakini navishukuru vyote kwa ujumla. Aidha, napenda kuwashukuru wote wanaoshirikiana nasi katika kutekeleza majukumu yetu kwa njia moja au nyengine; nawaomba waendelee kuwa nasi katika kufanikisha malengo ya kuwaletea wananchi maendeleo endelevu. Vile vile, nawashukuru kwa dhati Wanajamii, Wajasiriamali na Wawekezaji wote waliowekeza na wale wote walioonesha nia ya kuja kuwekeza nchini. Tunawakaribisha sana.

125. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua fursa hii adhimu kuwashukuru Watendaji wote wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuanzia Katibu Wakuu wa Uchumi na Uwekezaji pamoja na Katibu Mkuu anayesimamia Kazi na Uwezeshaji; Manaibu Makatibu Wakuu, Ofisa Mdhamini Pemba; Mkurugenzi Mtendaji ZIPA; Mkurugenzi Mtendaji ZEEA; Makamishna; Wakurugenzi, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi zilizopo chini ya Afisi na Watendaji wote kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi. Nakiri mbele yako kwamba mafanikio haya yaliyopatikana ni kwa juhudi zao

kubwa wanazifanya katika kufikia malengo tulijiwekea. Nawaomba waimarishe umoja na mshikamano tulionao katika kuwahudumia wananchi wetu na wawekezaji nchini.

126. **Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji napenda kuchukua fursa hii kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe na Wajumbe wote wa Baraza na Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa Miongozo, hekima, busara na maoni mnayotupatia katika kuimarisha utendaji wa shughuli zetu za kila siku. Nakuomba wewe na Wajumbe wako kuwa Mabalozi wazuri kwa Wananchi kuwashajiisha na kuhakikisha wananufaika na huduma mbali mbali tunazozitoa ikiwemo fursa za uwezeshaji, uwekezaji, ajira, mikopo na mafunzo ili waweze kuimarisha shughuli zao za kujipatia kipato na kuchangia katika kukuza uchumi wa Nchi. Mwisho napenda kumshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

127. **Mheshimiwa Spika; Naomba kuwasilisha.**

**MHE. SHARIFF ALI SHARIFF (MBM) WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS, KAZI,UCHUMI NA UWEKEZAJI**
**ZANZIBAR.**

VIAMBATANISHO

UKUAJI WA SEKTA YA UWEZESHAJI, UWEKEZAJI NA KAZI

Kiambatanisho nambari 1(a na b)AJIRA ZA NDANI






Kiambatanisho Nambari 2 a(i)

**FEDHA ZILIZOTOLEWA NA WANUFAIKA KUPITIA MKOPO WA INUKA JULAI,2023 – MACHI, 2024**

| | MIKOPO ILIYOTOKA | KIWANGO | ME | KE | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| | **UNGUJA** | | | | |
| 1 | KASKAZINI 'A' | 324,199,999.80 | 38 | 40 | 78 |
| 2 | KASKAZINI 'B' | 200,922,328.20 | 40 | 75 | 115 |
| 3 | KATI | 220,270,000 | 8 | 9 | 17 |
| 4 | KUSINI | 57,000,000 | 1 | 3 | 4 |
| 5 | MAGHARIBI 'A' | 609,647,747.09 | 79 | 116 | 195 |
| 6 | MAGHARIBI 'B' | 1,233,019,939.59 | 116 | 133 | 249 |

| | MIKOPO ILIYOTOKA | KIWANGO | ME | KE | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| 7 | MJINI | 3,911,900,000 | 387 | 179 | 566 |
| | **JUMLA UNGUJA** | **6,556,960,014.68** | **669** | **555** | **1224** |
| 1 | MICHEWENI | 304,866,444.80 | 158 | 125 | 283 |
| 2 | WETE | 614,600,000 | 230 | 209 | 439 |
| 3 | CHAKECHAKE | 438,454,460 | 35 | 40 | 75 |
| 4 | MKOANI | 36,083,222.40 | 11 | 13 | 24 |
| | **JUMLA PEMBA** | **1,394,004,127.20** | **434** | **387** | **821** |
| | **JUMLA KUU** | **7,950,964,141.88** | **1,103** | **942** | **2,045** |

Kiambatanisho Nambari 2 a(ii)

## MAREJESHO YA MIKOPO KUPITIA PROGRAMU 3 KUANZIA JULAI 2023 -MACHI 2024

| Programu | Inuka | | |
|---|---|---|---|
| | Makisio | Halisi | Asilimia |
| UNGUJA | 4,789,086,575 | 3,419,298,865 | 71% |
| PEMBA | 3,419,281,325 | 1,959,200,185 | 57% |
| **JUMLA** | **8,208,367,900** | **5,378,499,050** | **66%** |

| Programu | Mfuko wa Uwezeshaji | | |
|---|---|---|---|
| | Makisio | Halisi | Asilimia |
| UNGUJA | 167,532,925 | 6,720,000 | 4% |
| PEMBA | 50,367,025 | 7,114,000 | 14% |
| **JUMLA** | **217,899,950** | **13,834,000** | **6%** |

| Programu | Mboga mboga | | |
|---|---|---|---|
| | Makisio | Halisi | Asilimia |
| UNGUJA | 43,380,500 | 7,280,000 | 17% |
| PEMBA | 30,351,650 | 6,342,500 | 21% |
| **JUMLA** | **73,732,150** | **13,622,500** | **18%** |

Kiambatanisho nambari 2a (iii)

## FEDHA ZA PROGRAMU YA MAKUNDI MAALUM (4.4.2) ZILIZOPOKELEWA KUTOKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA.

| WILAYA | KIWANGO JULAI 2023 – MACHI 2024 | JUMLA KUANZIA MEI 2022 |
|---|---:|---:|
| KASKAZINI 'A' | 127,521,162.62 | 272,694,524.35 |
| KASKAZINI 'B' | 49,078,815.20 | 248,590,130.09 |
| KATI | 19,253,185.30 | 223,436,147.84 |
| KUSINI | 63,234,925.70 | 170,479,057.20 |
| MAGHARIBI 'A' | 127,247,830 | 187,282,699 |
| MAGHARIBI 'B' | 65,762,226 | 322,562,700 |
| MJINI | 0 | 384,000,000 |

| WILAYA | KIWANGO JULAI 2023 – MACHI 2024 | JUMLA KUANZIA MEI 2022 |
|---|---:|---:|
| MICHEWENI | 15,313,846.50 | 68,280,040.30 |
| WETE | 20,593,229 | 77,988,964 |
| CHAKECHAKE | 37,551,607 | 130,167,564 |
| MKOANI | 27,898,040.70 | 83,474,445.20 |
| JUMLA | 553,454,868.02 | 2,168,956,271.98 |

Kiambatanisho nambari 2(b)

IDADI YA VYAMA VYA USHIRIKA VILIVYOSAJILIWA



Kiambatanisho nambari 3(a, b na c)

## IDADI YA MIRADI YA UWEKEZAJI ILIYOIDHINISHWA




MIRADI LIYOIDHINISHWA KWA MITAJI (USD)
700,000,000
600,000,000
500,000,000
400,000,000
300,000,000
200,000,000
100,000,000
-
JUL
AUG
SEPT
OCT
NOV
DIS
JAN
FEB
2022/2023
2023/2024


MIRADI ILIYOIDHINISHWA KWA AJIRA
1600
1400
1200
1000
800
600
400
200
0
JUL
AUG
SEPT
OCT
NOV
DIS
JAN
FEB
2022/2023
2023/2024

## Kiambatanisho Nambari 4(a) FUNGU

## A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)

# MUHTASARI WA MAPATO YALIYOKUSANYWA KWA KIPINDI CHAJULAI 2023 HADI MACHI 2024

| NAMBARI YA KASMA | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO KWA MWAKA | MAKADIRIO KWA MIEZI TISA (JULY-MACHI) | MAKUSANYO HALISI (JULY-MACHI) | ASILIMIA YA MAPATO KWA MWEZI | ASILIMIA YA MAPATO KWA MWAKA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1422012 | Ada ya Uhakiki wa mikataba | 130,000,000 | 79,500,000 | 401,161,791 | 505% | 308.59% | Kuongezeka kwa ukaguzikazi katika maeneo ya kazi |
| | Ada ya vibali vya kazi kwa wataalamu wa kigeni | 1,710,161,000 | 1,243,843,376 | 3,066,945,090.8 | 247% | 179.34% | Mabadiliko ya ada ya vibali vya kazi yamepelekea kuongezeka kwa mapato |
| 1422071 | Ukaguzi wa Usalama naAfya maeneo ya Kazi | 420,000,000 | 310,000,000 | 174,693,600 | 56% | 41.59% | Upungufu wa vitendea kazi na,wafanyakazi katika idara ya osh imepelekea kupungua kwaukusanyaji wa mapato |
| 1422075 | Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi | 100,000,000 | 77,000,000 | 132,725,000 | 172% | 132.73% | Ongezeko la ajira kutoka nchi za njekumepelekea |
| | Ada ya Usajili wa Vyama Vya Ushirika | 90,000,000 | 69,000,000 | 23,950,000 | 35% | 26.61% | Kutokana na mahitaji halisi ya wananchi walioomba kusajiliwa |
| 1422037 | Ada ya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika | 60,000,000 | 46,500,000 | 18,148,767 | 39% | 30.25% | Uhamisho wa watendaji imepelekea kutofikia kiwango halisi kilichopangwa |
| | **JUMLA NDOGO** | **2,510,161,000** | **1,825,843,376** | **3,817,624,248.8** | **209%** | **152.09%** | |
| 1422012 | Ada ya Uhakiki wa mikataba | 40,000,000 | 33,500,000 | 5,065,000 | 15% | 12.66% | Upungufu wa wawafanyakazi imepelekea kupunguza wapato kama ilivyopangwa |
| 1422071 | Ukaguzi wa Usalama na Afya maeneo ya Kazi | 80,000,000 | 60,500,000 | 53,670,000 | 89% | 67.09% | Miradi mipya imesajiliwa kwa mwaka huu |
| 1422036 | Ada ya Usajili wa Vyama Vya Ushirika | 60,000,000 | 33,000,000 | 26,159,500 | 79% | 43.60% | Kutokana na mahitaji halisi ya wananchi walioomba kusajiliwa |
| 1422037 | Ada ya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika | 40,000,000 | 30,000,000 | 14,324,200 | 48% | 35.81% | Uhamisho wa watendaji imepelekea kutofikia kiwango halisi kilichopangwa |
| | **JUMLA NDOGO** | **220,000,000** | **157,000,000** | **99,218,700** | **63%** | **45.10%** | |
| | **JUMLA KUU** | **2,730,161,000** | **1,982,843,376** | **3,916,842,948.80** | **198%** | **143.47%** | |

Kiambatanisho Nambari 4b(i) FUNGU

AO7 (KAZI NA UWEZESHAJI)

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI NA MATUMIZI KWA MISHAHARA, RUZUKU, MATUMIZI YAKAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI, 2023- MACHI, 2024

| MAELEZO | BAJETI YA MWAKA YA AWALI 2023/2024 | BAJETI YA MWAKA BAADA YA UHAULISHO 2023/2024 | MAKADIRIO JULAI HADI MACHI 2023/2024 | MATUMIZI HALISI JULAI HADI MACHI 2023/2024 | ASILIMIA YA MAKADIRIO JULAI HADI MACHI 2023 /2024 | ASILIMIA YA MWAKA BAADA YA UHAULISHO 2023/2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| MISHAHARA YA KAWAIDA | 3,145,405,640 | 3,187,927,221 | 2,315,723,489 | 2,315,723,489 | 100 | **73** |
| MISHAHARA YA RUZUKU | 1,085,500,000 | 1,240,398,457 | 800,375,323 | 800,375,323 | 100 | **65** |
| **JUMLA NDOGO (A)** | **4,230,905,640** | **4,428,325,678** | **3,116,098,812** | **3,116,098,812** | **100** | **70** |
| MATUMIZI YA KAWAIDA (OC) | 1,993,700,000 | 1,992,188,128 | 1,635,214,751 | 690,000,499 | 42 | **35** |
| MATUMIZI YA RUZUKU (SO) | 1,699,000,000 | 812,900,000 | 649,990,800 | 487,357,620 | 75 | **60** |
| **JUMLA NDOGO (B)** | **3,692,700,000** | **2,805,088,128** | **2,285,205,551** | **1,177,358,119** | **52** | **42** |
| MIRADI YA MAENDELEO **(C)** | 7,040,605,580 | - | - | - | 0 | |
| JUMLA KUU (A+B+C ) | 14,964,211,220 | 7,233,413,806 | 5,401,304,363 | 4,293,456,931 | 79 | 59 |

TANBIHI:

| UHAULISHO (VIREMENT) WA BAJETI YA SMIDA | "TZS" |
|---|---:|
| BAJETI YA FEDHA ZA MAENDELEO ZA SMIDA JUMLA | 7,040,605,580 |
| BAJETI YA FEDHA ZA RUZUKU YA SMIDA JUMLA | 1,366,105,640 |
| **JUMLA YA BAJETI KIFUNGU CHA SMIDA** | **8,406,711,220** |
| BAJETI baada ya kutoka SMIDA | 6,557,500,000 |
| Realocation salary (TOPING UP FROM SALARY ADJUSTMENT) | 675,913,806 |

Kiambatanisho Nambari 4b(ii) FUNGU

A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHAJULAI, 2023-MACHI, 2024

| PROGRAMU | BAJETI YA MWAKA 2023/2024 | BAJETI YA MWAKA (BAADA YA UHAULISHO) | MAKADIRIO YA MIEZI TISA(JULAI 2023-MACHI 2024) | MATUMIZI MENGINEYO (OC) "A" | MATUMIZI YA MISHAHARA NA RUZUKU YA MSHAHARA "B" | JUMLA YA FEDHA ZILIZOINGIZWA (JULAI 2023 – MACHI 2024)"A+B" | ASILIMI AYA FEDHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 (%) | ASILIMI AYA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1. PROGRAMUKUU YA USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI** | **1,738,400,000** | **1,893,298,457** | **1,329,555,123** | **385,397,700** | **800,375,323** | **1,185,773,023** | **89** | **63** |
| Kamisheni ya kazi | 1,348,400,000 | 1,503,298,457 | 999,915,123 | 171,945,800 | 800,375,323 | 972,321,123 | 97 | 65 |
| Idara ya Usalama na Afya Kazini | 190,000,000 | 190,000,000 | 146,275,000 | 76,911,500 | - | 76,911,500 | 53 | 40 |
| Idara yaAjira | 200,000,000 | 200,000,000 | 183,365,000 | 136,540,400 | - | 136,540,400 | 74 | 68 |
| **2. PROGRAMU KUU YA UWEZESHAJI WANANCHI** | **10,766,374,220** | **2,455,255,139** | **1,933,119,740** | **434,259,417** | **969,683,239** | **1,403,942,656** | **73** | **57** |

| KIUCHUMI | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfuko wa Uwezeshaji (WAKALA) | 608,241,000 | 608,241,000 | 637,604,305 | 101,959,920 | 516,793,305 | 618,753,225 | 97 | 102 |
| SMIDA | 8,406,711,220 | - | - | 54,756,880 | - | 54,756,880 | | |
| Idara ya Maendeleo ya Ushirika | 873,374,000 | 890,220,139 | 662,523,010 | 100,696,362 | 299,428,009 | 400,124,371 | 60 | 45 |
| Uwezeshaji Kiuchumi (WAKALA) | 878,048,000 | 956,794,000 | 632,992,425 | 176,846,256 | 153,461,925 | 330,308,181 | 52 | 35 |
| 3. PROGRAMU | | | | | | | | |
| [illegible] na Utafiti | | | | | | | | |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] |
| Afisi Kuu Pemba | [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] |
| JUMLA KUU | 14,964,211,220 | 7,233,413,806 | 5,401,304,363 | 1,177,358,119 | 3,116,098,812 | 4,293,456,931 | 79 | 59 |

Kiambatanisho 4c(i)

FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI NA MATUMIZI KWA MISHAHARA, RUZUKU, MATUMIZI YAKAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI, 2023 – MACHI, 2024

| ENEO | BAJETI ILIYOIDHINISHWA MWAKA 2023/2024 | BAJETI YA MAREKEBISHO MWAKA 2023/2024 | MAKADIRIO JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | MATUMIZI JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | ASILIMIA YA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | ASILIMIA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| MISHAHARA | 770,100,000 | 945,253,288 | 602,671,654 | 564,123,853 | **94** | **60** |
| RUZUKU YA MSHAHARA | 2,887,800,000 | 3,697,800,000 | 2,705,850,000 | 2,675,423,010 | **99** | **72** |
| MATUMIZI YA KAWAIDA | 1,074,300,000 | 1,074,300,000 | 843,840,000 | 366,850,000 | **43** | **34** |
| MIRADI YA MAENDELEO | 3,500,000,000 | 13,195,346,041 | 11,445,364,560 | 9,695,364,560 | **85** | **74** |
| **JUMLA** | **8,232,200,000** | **18,912,698,329** | **15,597,726,214** | **13,301,761,423** | **85** | **70** |

Kiambatanisho Nambari 4c(ii)

FUNGU A08 ( UCHUMI NA UWEKEZAJI)

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHAJULAI, 2023- MACHI, 2024

| PROGRAMU | BAJETI YA MWAKA 2023/2024 | MAKADIRIOYA MIEZI TISA | FEDHA ZILIZO INGIZWA (OC) "A" | FEDHA ZA MAENDELEO ZILIZO INGIZWA "B" | FEDHA ZILIZOINGIZWA (MSHAHARA NA RUZUKU YA MSHAHARA) "C" | JUMLA YA FEDHA ZILIZO INGIZWA "A+B+C" | ASILIMIA YA FEDHA ZILIZO INGIZWA YA MIEZI TISA | ASILIMIA YA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PA0801: Programu Kuu ya Kushajiisha Uwekezajina Mashirikianobaina Sekta ya Umma na Sekta Binafsi** | **17,378,822,241** | **14,515,418,376** | **63,300,000** | **9,695,364,560** | **2,773,204,775** | **12,531,869,335** | **86.33** | **72.11** |
| Program ya Maendeleo ya Uimarishaji wa Maendeo Huru ya Uwekezaji | 13,195,346,041 | **11,445,364,560** | **-** | 9,695,364,560 | **-** | 9,695,364,560 | **84.71** | **73.48** |
| Programu Ndogo ya Kushajiisha Uwekezaji wa ndani na Nje ya Nchi | 3,697,800,000 | **2,705,850,000** | - | - | 2,675,423,010 | 2,675,423,010 | **98.88** | **72.35** |
| Programu Ndogo ya Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi | 485,676,200 | **364,203,816** | 63,300,000 | | 97,781,765 | 161,081,765 | **44.23** | **33.17** |
| **PA0802: Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibuwa Afisi ya Rais, Kazi,** | **1,533,876,088** | **1,082,307,838** | **303,550,000** | | **466,342,088** | **769,892,088** | **71.13** | **50.19** |

Kiambatanisho Nambari 5

## PROGRAMU KUU NA NDOGO ZA AFISI YA RAIS KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI KWA FUNGU A07(KAZI NA UWEZESHAJI), FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI) NA FUNGU A11 (UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI)

*Jadweli nambari 1 - FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)*

| |
|---|
| PA0702: Programu Kuu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote. |
| SA070201: Programu Ndogo ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha. |
| SA070202: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini. |
| SA070203: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini |
| SA070203: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini |
| PA0703: Programu Kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. |
| SA070302: Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika |
| PA0705: Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji. |
| SA070501: Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi |
| SA070502: Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji |
| SA070503: Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba |

*Jadweli nambari 2: FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)*

| |
|---|
| PA0801: Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi |
| SA080101: Programu Ndogo ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi |
| SA080102: Programu Ndogo ya Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji |
| PA0802: Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji. |
| SA080201: Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji |
| SA080202: Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi |
| SA080203: Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba |

*Jadweli nambari 3 – FUNGU A11 (UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI)*



| |
|---|
| PA1101: Programu Kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi |
| SA110101: Programu Ndogo ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi |
| PA1102: Programu Kuu ya Uendeshaji na Utawala wa Taasisi ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi |
| SA110201: Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji |
| SA110202: Programu Ndogo ya Afisi ya Uratibu Pemba |

Kiambatanisho Nambari 6

## MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

| PEMBA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **KASMA** | **MAELEZO** | **MAKADIRIO 24-25** | **MAKADIRIO 25-26** | **MAKADIRIO 26-27** |
| 1422012 | Uthibitisho wa mikataba ya kazi | 12,000,000 | 15,000,000 | 20,000,000 |
| 1422071 | Ukaguzi katika maeneo ya kazi | 226,191,422 | 355,000,000 | 380,000,000 |
| 1422036 | Usajili wa vyama vya ushirika | 50,000,000 | 70,000,000 | 80,000,000 |
| 1422037 | Ukaguzi wa vyama vya ushirika | 40,000,000 | 90,000,000 | 100,000,000 |
| **JUMLA PEMBA** | | **328,191,422** | **530,000,000** | **580,000,000** |
| **UNGUJA** | | | | |
| **KASMA** | **MAELEZO** | **MAKADIRIO 24-25** | **MAKADIRIO 25-26** | **MAKADIRIO 26-27** |
| 1422012 | Uthibitisho wa mikataba ya kazi | 388,100,000 | 394,000,000 | **400,000,000** |
| 1422011 | Vibali vya kazi kwa wataalamu wa kigeni | 4,484,128,578 | 4,545,256,895 | **5,000,000,000** |
| 1422075 | Ada ya ukaguzi wa miktaba ya ajira nje ya nchi | 245,000,000 | 300,000,000 | **350,000,000** |
| 1422071 | Ukaguzi katika maeneo ya kazi | 1,000,000,000 | 1,100,000,000 | **1,200,000,000** |
| 1422036 | Usajili wa vyama vya ushirika | 150,000,000 | 200,000,000 | **2,100,000,000** |
| 1422037 | Ukaguzi wa vyama vya ushirika | 100,000,000 | 110,000,000 | **120,000,000** |
| **JUMLA UNGUJA** | | **6,367,228,578** | **6,649,256,895** | **9,170,000,000** |
| **JUMLA KUU** | | **6,695,420,000** | **7,179,256,895** | **9,750,000,000** |

Kiambatanisho Nambari 7 a

## MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA AFISI YA RAIS KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJIKWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

| PROGRAMU | MATUMIZI YA KAWAIDA "000" | MISHAHARA "000" | RUZUKU YA OC "000" | RUZUKU YA MISHAHARA "000" | MAENDELEO SMZ "000" | MAENDELEO WADAU "000" | JUMLA "000" |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| FUNGU A07 | 2,193,000 | 2,902,300 | 848,800 | 1,329,200 | | | **7,273,300** |
| FUNGU A08 | 1,595,800 | 811,500 | - | 3,645,800 | 15,000,000 | | **21,053,100** |
| FUNGU A11 | 2,022,000 | 1,257,700 | | | 36, 500,000 | 7,100,000 | **46,879,700** |
| **JUMLA KUU** | **5,810,800** | **4,971,500** | **848,800** | **4,975,000** | **51,500,000** | **7,100,000** | **75,206,100** |

Kiambatanisho Nambari 7 b

## MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA AFISI YA RAIS KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJIKWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025



Kiambatanisho Nambari 8 a

## MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 KWA FUNGU LA A07(KAZI NA UWEZESHAJI)

| PROGRAMU | MATUMIZI YA KAWAIDA | MISHAHARA | RUZUKU YA OC | RUZUKU YA MISHAHARA | MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu kuu ya usimamizi wa Sheria za kazi, Ukaguzi kazi na Kazi za staha kwa wote** | - | - | **848,800,000** | **1,329,200,000** | - | **2,178,000,000** |
| Programu ndogo ya uratibu wa upatikanaji wa Ajira za Staha | | | 260,000,000 | | | **260,000,000** |
| Programu ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini | | | 247,020,000 | | | **247,020,000** |
| Programu ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja | | | 341,780,000 | 1,329,200,000 | | **1,670,980,000** |
| **Programu kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi** | **615,200,000** | **465,525,000** | - | | - | **1,080,725,000** |
| Programu ndogo ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | | | | | | - |
| Programu ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika | 615,200,000 | 465,525,000 | | | | **1,080,725,000** |
| Programu ndogo ya uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | | | | | | - |
| **Programu kuu ya Uendeshajina Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji** | **1,577,800,000** | **2,436,775,000** | | - | | **4,014,575,000** |
| Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti | 370,100,000 | 233,787,000 | | | | **603,887,000** |
| Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji | 657,000,000 | 1,466,014,000 | | | | **2,123,014,000** |
| Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba | 550,700,000 | 736,974,000 | | | | **1,287,674,000** |
| JUMLA KUU | 2,193,000,000 | 2,902,300,000 | 848,800,000 | 1,329,200,000 | | 7,273,300,000 |

Kiambatanisho Nambari 8 b

## MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 KWA FUNGU LA A11 (WAKALA WA UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI)

| Programu | Matumizi ya kawaida | Mshahara | Mchango wa SMZ | Washirika wa Maendeleo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Programu kuu ya kuwawezesha wanachi kuchumi** | **567,125,000** | **-** | **36, 500,000,000** | **7,100,000,000** | **44,167,125,000** |
| Programu ndogo ya Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi | 567,125,000 | - | 36, 500,000,000 | 7,100,000,000 | 44,167,125,000 |
| **Programu Kuu ya Utumishi na Uendeshaji wa Taasisi ya ZEEA** | **1,454,875,000** | **1,257,700,000** | **0** | | **2,712,575,000** |
| Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji | 955,275,000 | 1,029,942,000 | 0 | | 1,985,217,000 |
| Programu ya Afisi Kuu Pemba | 499,600,000 | 227,758,000 | 0 | | 727,358,000 |
| **Jumla** | **2,022,000,000** | **1,257,700,000** | **36, 500,000,000** | **7,100,000,000** | **46,879,700,000** |

Kiambatanisho Nambari 8 c

## MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 KWA FUNGU LA A08(UCHUMI NA UWEKEZAJI)

| PROGRAMU | MATUMIZI YA KAWAIDA | MISHAHARA | RUZUKU YA OC | RUZUKU YA MISHAHARA | MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu kuu ya kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano baina ya sektaya Umma na Sekta binafsi** | **634,830,000** | **127,238,400** | | **3,645,800,000** | **15,000,000,000** | **19,407,868,400** |
| Programu ndogo ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi | 634,830,000 | 127,238,400 | | | | **762,068,400** |
| Programu ndogo ya Maendeleo ya Uchumi kupitia Uwekezaji | | | | 3,645,800,000 | 15,000,000,000 | **18,645,800,000** |
| **Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu waAfisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji** | **960,970,000** | **684,261,600** | | | | **1,645,231,600** |
| Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti | 342,380,000 | 93,470,600 | | | | **435,850,600** |
| Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji | 465,590,000 | 557,812,000 | | | | **1,023,402,000** |
| Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba | 153,000,000 | 32,979,000 | | | | **185,979,000** |
| **JUMLA KUU** | **1,595,800,000** | **811,500,000** | | **3,645,800,000** | **15,000,000,000** | **21,053,100,000** |



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi akipata maelezo kutoka kwa mmoja wa Wafanyabiashara waliohudhuria katika Tamasha la Fahari ya Zanzibar ya maadhimisho ya mwaka mmoja wa ZEEA katika Hoteli ya Golden Tulip Uwanja wa Ndege



Ugeni kutoka Shirika la Kazi Duniani (ILO) ukiongozwa na Mkurugenzi wa Shirika hilo kanda ya Afrika Bi. Fanfan Rwanyindo Kayirangwe (wa pili kushoto) wakipatiwa zawadi na Katibu Mkuu (Kazi na Uwezeshaji) Bi. Maryam Juma Abdulla pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara Maendeleo ya Viwanda Bi Fatma Mbarouk, baada ya kufanya mazungumzo na ugeni huo Mwanakwerekwe Wilaya ya Magharibi B.